

ALIYE MKUU KULIKO

SULEMANI YUPO HAPA SASA



Na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tu, tunaposoma Neno la Bwana. Ninyi ambao mngetaka kufungua kwenye somo la Maandiko, usiku wa leo, fungueni Mathayo 12, kuanzia aya ya 38.

Na pale, hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona.

Kwani kama vile Yona aliyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

² Na tuinamishe vichwa vyetu. Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa katika Uwepo Wake, je! kuna ombi hapa ndani usiku wa leo, ambalo ungetaka likumbukwe katika maombi? Kama lipo, inueni tu mikono yenu, na uonyeshe kwa kufanya hivyo, “Mungu, sikia ombi langu.” Sasa omba kimoyoyo tunapoingia katika maombi.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tuyahesabu haya ni moja ya majaliwa mazuri sana tuliyo nayo upande huu wa Utukufu, ni kukutana katika kusanyiko la watu wanaokuamini Wewe, ambapo tunaweza kutarajia Uwepo Wako, kwa sababu ni kulingana na ahadi Yako. Ulisema, “Mahali walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, niko katikati yao. Na ikiwa wanaweza kukubaliana juu ya jambo lo lote, na kuomba, watalipokea.” Bwana, jambo kubwa sana tunaloweza kukubaliana, usiku wa leo, ni kwamba ukutane nasi tu, tupate kuuona Uwepo Wako, tuuhisi Huo katika roho zetu, na tujue ya

kwamba Wewe uko hapa. Na katika Uwepo Wako, tunajisikia ya kwamba tunaweza kuimimina mioyo yetu, katika maombi. Nasi tunapokutafakari Wewe, naomba tusikie hisi hii kubwa ya kujibiwa kwa maombi yetu, kwa kuwa tunaomba sasa katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

⁴ Ninataka kuchukua somo, Bwana akipenda, pamoja na Maandiko niliyoandika hapa, kwa muda kidogo tu kabla hatujaingia katika kuwaombea wagonjwa, juu ya somo la: *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa Sasa*.

⁵ Tunaona katika mwanzo wetu wa Maandiko usiku wa leo, mahali ambapo somo letu linapatikana, ya kwamba Yesu alikuwa akishindana na Mafarisayo. Alikuwa akiwakemea, kwa sababu hawakuwa wamemfahamu Yeye. Mtu, ambaye wanatheolojia waliokuwa wamefunzwa, wakiutazamia wakati wa kuonekana Kwake, na halafu, wakati alipowasili, walimwelewa vibaya na wakawa wamemwita Yeye, “pepo.” Walisema ya kwamba huduma aliyokuwa nayo ilikuwa ni ya Ibilisi, kwa kuwa aliweza kuyatambua mawazo yaliyokuwa mioyoni mwao, na kwa jambo hili walimfikiria Yeye kwamba ni aina fulani ya—ya mchawi ama kitu kama mpiga ramli; na mtu ye yote anajua hao ni pepo wachafu. Halafu basi, kuita kazi ya Mungu, “pepo mchafu,” ilikuwa ni kukufuru.

⁶ Naye alikuwa amewaambia angewasamehe jambo hilo, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa hajaja bado kuifanya mioyo yao myororo na—na kuwaweka katika hali ambayo kwamba wanguweza kumfahamu Mungu. Mioyo yao ilikuwa mbali sana na Mungu. Yote waliyojua ilikuwa ni theolojia baridi ya torati, wala hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu. Lakini Yeye alisema, “Roho Mtakatifu akiisha kuja na kufanya jambo lile lile, kusema neno juu Yake, halitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ule ujao.”

⁷ Nami nilikuwa nikifikiri nilipokuwa nikisoma jambo hili, alasiri ya leo, na kulitafakari, jinsi ambavyo kwamba—kwamba wao, mmoja wao hapa, alimjia, katika njia ya kumzunguka, na kumwuliza, akasema, “Bwana, twataka kuona ishara Kwako.” Katika maneno mengine, Wayahudi daima walifunzwa kuamini ishara. Wayahudi hutafuta ishara, daima; na Wayunani hekima. Nasi tunaona ya kwamba Wayahudi hawa walikuwa wakitegemea ishara.

⁸ Sasa, ni—ni ushuhuda wa jinsi gani dhidi ya Farisayo huyu, kwamba yeyee alidhaniwa anajua Maandiko, ya kwamba ishara ya Masihi, Yesu alikuwa ameisha itenda, na macho yake yalikuwa yametiwa giza sana hata hakuweza kutambua jambo hilo. Yesu alikuwa, Yesu alikuwa amempa ishara ya kweli ya Masihi ya Kimaandiko iliyoahidiwa katika Maandiko. Lakini alikuwa yeye akitafuta ishara ya namna nyingine.

9 Na jinsi jambo hilo lilivyo la kweli kuwahusu waalimu wa siku hizi, na watu wa siku hizi. Wao wanaweza kuona jambo fulani lililo thabiti na liko kwenye Maandiko, lililoahidiwa na Mungu, kwa siku hii. Na basi wanaweza kuona jambo Hilo, lakini hata hivyo wao wanatazamia jambo fulani la usoni, wanataka kuona jambo lingine, na wanaacha ishara ya zamani hizi.

10 Yeye alikuwa amewaambia wakati mmoja, kasema, “Mnaweza kuutambua uso wa mbingu wakati zinatanda, ni nyekundu. Mtasema, wakati zinatanda na ni nyekundu, ‘kesho kutakuwa na dhoruba,’ na kadhalika.” Lakini kasema, “Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, lakini, ishara za zamani hizi, hamzifahamu.” Kwa kuwa ni kweli Maandiko yalikuwa yamesema ya kwamba Masihi huyu atakuwa ni nabii.

11 Tunajua ya kwamba njia ya Mungu ya kufanya mambo daima ilikuwa ni kumtuma nabii kuthibitisha ujumbe Wake. Kamwe haijashindwa. Haitashindwa kamwe. Mungu hawezi kubadilisha njia Zake. Vile uamuzi Wake wa kwanza ulivyo, hauna budi kubaki hivyo daima. Anayosema ni kweli.

12 Mungu kamwe hajajishughulisha na makundi makubwa. Yeye daima hushughulika na mtu binafsi. Hivyo ndivyo alivyowachukua watu kutoka katika Mataifa kwa ajili ya Jina Lake; mtu binafsi tu, mmoja hapa na mwingine pale, kwa ajili ya Jina Lake. Yeye hushughulika na mtu binafsi, si makundi.

13 Nasi tunaona ya kwamba sababu ya wao kuamini jambo hili, ya kwamba nabii hana budi kuwa ni shahidi wa Mungu aliyethibitishwa. Kwa maana aliposema jambo lo lote, nalo likatimia; na akasema tena, nalo likatimia; na lo lote alilosema, Mungu alilithibitisha kwamba ni kweli, basi Yeye alisema, “Msikieni, kwa maana Mimi niko pamoja naye.”

14 Sasa tunaona ya kwamba Musa, ambaye wao walidai wanamwamini, alikuwa amewaambia ya kwamba, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii aliye kama mimi, na Huyu watu hawana budi kumsikia. Na wote ambao hawakumsikia Nabii huyu watakatiliwa mbali na watu.”

15 Tunaona jambo hilo kwamba ni kweli. “Alikuwa Kwake; walio Wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.”

16 Jinsi tunavyoona Mafarisayo hawa wakiangalia moja kwa moja, na Masadukayo, kwenye yale hasa ahadi ya Mungu iliyosema ya kwamba Yeye angefanya. Na wao walikuwa tu hapo bado wakitaka ishara, bila kujua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya kweli ya Masihi aliyokuwa aonyeshe.

17 Filipino aliifahamu, wakati Yeye alipomwambia mahali alipokuwa siku iliyotangulia. Yeye alifahamu ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, kasema, “Wewe ndiwe Kristo, na Wewe

ni Mfalme wa Israeli.” Na kwa hiyo yeye—yeye alitambua jambo hilo kwa sababu alikuwa amejitolea kwalo. Alikuwa amejitolea.

¹⁸ Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watanjia Mimi.” Haidhuru tujaribu jinsi gani kwa njia nyingine yo yote, haina budi kuwa Mungu. “Si katika uwezo wake yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio, ni Mungu arehemuye.” Mungu Ndiye anayechagua. “Ninyi hamkunichagua Mimi,” kasema Yesu, “Mimi niliwachagua ninyi.”

¹⁹ Na sasa tunaona ya kwamba yule mpinga-Kristo, katika siku ya mwisho, “atawadanganya wote wakao juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Jina lako liliwekwa katika Kitabu cha Mungu kabla Mwana-Kondoo hajachinjwa. Wakati mpango Wake ulipoamuriwa, kila kitu, wewe ulitambuliwa katika mpango huo kwa sababu una Uzima wa Milele. Neno *Milele*, haikuwa na mwanzo na wala haiwezi kukoma, nawe ni sifa za mawazo ya Mungu kabla ulimwengu haujaumbwa. Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kupata Uzima wa Milele. Na Uzima huo, ambao Yeye alikuwa akikufikiria, umo ndani yako sasa. Hakuna njia ya kuutenganisha. Unakaa hapo ndani.

²⁰ Angalia sasa, hawa Mafarisayo, ingawa walikuwa waalimu wa dini, wasomi mashuhuri wa theolojia, na walikuwa wamekisoma Kitabu, usiku na mchana, walishindwa kuiona hiyo ishara ya Masihi, nao walikuwa hapa wakijaribu kumtaka Yeye awape ishara.

²¹ Ili nipate kuendeleza jambo hili, kuwajulisha ya kwamba Mungu daima hutoa ishara. Kwa sababu Yeye ni mwenyezi, Yeye daima hushughulika na watu kwa ishara, ishara za Kimaandiko.

²² Katika Agano la Kale, wakati walipokuwa na—na swali, mtu fulani aliota ndoto, na hapakuwepo na—na nabii hapo, walimpeleka hekaluni, mahali walipokuwa na kile walichoita Urimu Thumimu. Ninyi waalimu wa Biblia mnafahamu ninayomaanisha. Ilikuwa ni kile—kile kifuko cha kifuani ambacho Haruni alivaa, ambacho kilikuwa na yale mawe kumi na mawili yaliyowakilisha makabila kumi na mawili ya Israeli. Wao walikitundika hicho kwenye nguzo; na halafu wakati nabii huyu, ama mwotaji huyu, ama ye yote yule, aliposimulia ono ama ndoto yake, haidhuru ilionekana ni halisi jinsi gani, kama hizo nuru za kimbinguni hazikumulika, zikifanya ile Urimu Thumimu kwenye kile kifuko cha kifuani, ilikataliwa. Mungu aliikataa.

²³ Hazina budi kuwa ni ishara ya kimbinguni kutoka kwa Mungu, kuthibitisha. Haidhuru ilikuwa ni halisi jinsi gani, ni ya kilindi jinsi gani katika theolojia, jinsi ilivyosikika kwamba

ni kuu, ingali hivyo, kama ishara ya kimbinguni ya Mungu haikuthibitisha hilo, hayo hayakuwa ni ya kweli, kwa Myahudi.

²⁴ Sasa, Agano la Kale, kile kifuko cha Haruni kiliondolewa pamoja na lile Agano la Zamani.

²⁵ Lakini katika Agano Jipya, Mungu angali ana Urimu Thumimu. Hiyo ni kusema, kama nabii, mwotaji, mwanatheolojia, ama cho chote kile, akinena jambo ambalo ni kinyume cha Neno, na Mungu asirudishe mwangwi wake kupitia kwenye Neno, nitaliachilia mbali, kwa sababu Hilo ndilo Urimu ya Thumimu ya Mungu. Nami ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote, ya kwamba ni Neno la Mungu.

²⁶ Na Mungu ni Neno Lake Mwenyewe. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno alikuwa pamoja na Mungu na Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu.” “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yuko hivyo, hata sasa. Mungu hahitaji mfasiri ye yote.

²⁷ Sisi tunafasiri, tunasema, “*Hili, hili* ni lile, na *hili* ni lile,” na kadhalika.

²⁸ Mungu hahitaji mfasiri ye yote. Yeye ndiye anayejifasiria. Mungu hatuhitaji sisi kulifasiri Neno Lake. Biblia, limeandikwa, Nalo linasema si la kufasiriwa anavyotaka mtu ye yote. Mungu alisema, hapo mwanzo, “iwe nuru,” ikawa nuru. Hiyo ndiyo fasiri yake. Mungu alisema, “bikira atachukua mimba,” naye akachukua mimba. Hiyo ndiyo fasiri yake. Haihitaji mtu ye yote kuifasiri.

²⁹ Mungu alisema, katika siku hii, mambo haya yangetukia, nayo yanatukia. Hayahitaji kufasiriwa ko kote. Ni Mungu akijifasiria Mwenyewe. Yanatukia. Haidhuru tujaribu kulivuruga jinsi gani, na kusema, “Halimaanishi *Hivi*, wala halimaanishi *Lile*.” Linamaanisha jambo lilo hilo hasa, na Mungu ndiye anayejifasiria Mwenyewe. Yeye huthibitisha Neno Lake, na hiyo ndiyo fasiri Yake, kwa sababu linatimizwa.

³⁰ Sasa tunaona hawa jamaa pale, katika Mathayo sura ya 12, aya ya 38 hadi 40, nao walikuwa wakimwuliza, “Mwalimu, twataka ishara kutoka Kwako.”

³¹ Naye alikuwa anawakemea kwa sababu hawakuwa wamemwamini, na walikuwa wamemwita Roho mwenyewe aliyekuwa juu Yake, “pepo mchafu,” katika kutokuamini kwao, kwa maana hawakuweza kumtambulisha Yeye miongoni mwa makasisi mwao—mwao. Hawakuweza kutambulisha (ninii Yake) mahali Yeye alipotoka. Hawakujua alitoka shule gani, kama alikuwa Mfarisayo ama Msadukayo; na daima alikuwa anakazana kuvivuruga vyo vyao vya—vya theolojia, na kuwaita kundi la “majoka.” Na, mbona, hawakuweza kumtambulisha na kundi lo lote. Na kwa hiyo, “Mtu huyu alitoka wapi? Hatujui anakotoka.” Wala hawakutambua ile ishara yenyewe hasa, ya kwamba alikuwa ndiye Masihi, alikuwa pale.

³² Sasa, kama yule maskini mwanamke pale kisimani, tuliyenena habari zake majuzi usiku. Yeye alitambua jambo hilo, nalo likamfanyia jambo fulani. Na wale waliotambua jambo—jambo hilo, hao ndio waliokuwa uzao wa Mungu ulioitwa katika siku hiyo.

³³ Mungu, na daima katika nyakati zote, daima amewapa watu Wake karama za kiroho. Hivyo ndivyo anavyotambulishwa na kujulikana, kwa karama za kiroho. Na hapo Mungu anapotuma karama ya kiroho kwa watu Wake, na karama hiyo ya kiroho inakataliwa, basi hao—watu hao huingia katika giza la machafuko. Kila wakati, katika nyakati zote, wakati Mungu anapowatumia watu jambo fulani, karama, nao wanalikataa, watu hao wanakataliwa na Mungu kwa sababu wameikataa rehema ya Mungu.

³⁴ Loo, ungekuwa ni usalama wa namna gani, usiku wa leo, jinsi lingekuwa ni jambo bora zaidi kuliko kinga zote za mabomu na—na mahali pote tungaliweza kuwazia, kama taifa hili, ambalo linaitwa taifa la Kikristo, lingeweza kukubali karama ya Mungu ambayo limepewa, Roho Mtakatifu aliye mkuu aliyemwagwa katika siku hizi za mwisho. Na jinsi ambavyo kama taifa hili lingekubali jambo Hilo, lingekuwa mahali pa salama zaidi kuliko kitu cho chote wangaliweza kuingia ndani yake. Lakini walimkataa, kwa hiyo hakuna kilichosalia ila machafuko na hukumu.

³⁵ Nyakati zote, Yeye alitoa hizi karama kuu za kiroho. Tena angalia daima kuja kwa karama ya kiroho, karama ya kweli; ninataka kunena habari zake, usiku mmoja, juu ya “Sauti ya karama,” lakini ni kama Bwana akipenda. Lakini sikuzote karama hizi kwa kawaida hutangazwa na manabii. Halafu unapomwona nabii akitokea jukwaani, hiyo inaonyesha ya kwamba hukumu i karibu. Sasa hiyo ni ishara, unapomwona nabii wa Mungu aliyethibitishwa akitokea jukwaani; katika siku za Yeremia, katika siku za Danieli, katika siku za—za Yohana Mbatizaji, katika siku za Bwana Yesu, na zamani zote. Nabii anapotokea jukwaani, ni wakati ambapo Mungu yuaenda kunena Neno Lake. Mataifa yanalikataa, na ndipo machafuko yanaingia.

³⁶ Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika kule kubadilika kwa nyakati za kanisa, kila wakati, wakati ujumbe ulipokataliwa. Na Mungu akitoa karama hizi na jumbe kwa watu, nao wanazikataa, basi hakuna kilichosalia ila hukumu.

³⁷ Mungu ni mwenye haki. Yeye hatatuma hukumu kabla hajatoa rehema. Na rehema inabashiriwa mbele na jinsi itakavyokuja, lakini watu kama ilivyo kawaida yake wamechanganyikiwa kabisa, na katika nia zao, na mipango mingi sana mbali mbali waliyojitengenezea, mpaka wanakosa kumtambua. Na hivyo ndivyo inavyotukia daima.

³⁸ Sasa tunaona ya kwamba Yeye aliwaambia ya kwamba, “Ki—kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara.” Ni mara ngapi asiyeamini amejinufaisha vibaya na jambo hili, kuhusu ishara za Kimaandiko, wala hawaziamini!

³⁹ Mungu daima hunena kwa ishara. Daima amefanya hivyo. Daima atafanya hivyo. Mradi tu kuna ulimwengu, Yeye atadumu akinena kwa ishara za kiroho. Yeye ametabiri zingekuja.

⁴⁰ Sasa wengi wa wasioamini wanachukua jambo hilo, wakati Yeye aliposema, “Kizazi kibaya na, ama, kizazi kidhaifu na cha zinaa kinatafuta ishara.”

⁴¹ Angalia, Yeye alikuwa akinena katika unabii ulio maradufu hapa. Alikuwa akiwaambia pia ya kwamba wao walikuwa ni kizazi kidhaifu na cha zinaa; na pia akiwaambia ya kwamba kizazi *cho chote* kidhaifu na cha zinaa, na kile ambacho kitakuja, kitapokea ishara. Angalia, Yeye alisema, “Kizazi kidhaifu na cha zinaa chatafuta ishara; wala hakitapewa ishara, ila ishara ya Yona. Kwani kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku.”

⁴² Yeye alikuwa akisema nini hapa? Alikuwa akisema, ya kwamba, “Kizazi kibaya na cha zinaa kingepokea ishara ya kufufuka.” Na ni wakati gani mwingine tumepata kuufikia, ulio zaidi ya ulivyo wa sasa hivi, wa kizazi kinachomkataa Kristo, kiovu, kilichopotoshwa, cha zinaa? Nao watapokea ishara, ishara ya ufufuo, ya kwamba Yesu Kristo yu hai usiku wa leo kama vile tu alivyowahi kuwa. Yeye amefufuka katika wafu, ikimfanya yeye yule jana, leo, na hata milele. “Kizazi kidhaifu na cha zinaa chatafuta ishara, nao wataipata, na ishara hiyo itakuwa ishara ya ufufuo.” Sasa, bila shaka, alikuwa akisema nao, ya kwamba yeye angefufuka katika wafu.

⁴³ Mara nyingi, Maandiko yana ninii yake ya kawaida, ama maana zake mbili. Kama vile katika Mathayo 3, ilivyosema, “Tli litimie neno lililonenwa na Bwana kwa nabii, akisema, ‘Kutoka Misri nilimwita Mwanangu.’” Sasa kama ukirejea huko nyuma, ni katika Hosea, naye alitabiri ya kwamba, “Kutoka Misri Yeye alimwita mwanawe, ambaye alikuwa ni Israeli.” Yakobo alikuwa mwana wa Mungu, Naye akamwita atoke Misri. Hapa ndipo ambapo marejeo yanakuelekeza. Lakini, pia, Kristo alikuwa Mwanawe aliye Mkuu zaidi, Naye akamwita atoke, Israeli ikiwa ni mfano.

⁴⁴ Na kwa hiyo huo ulikuwa ni mfano wa kumkataa Kristo, katika kizazi hicho; huyu ni mfano mkubwa zaidi, kwa maana kizazi kile kilichokataa kule kufufuka kilipata msamaha, lakini kizazi hiki kinachomfanyia mzaha Roho Mtakatifu hakisameheki. Sisi tuninii... Yeye anayemkataa Roho Mtakatifu ni mkuu kuliko yeye anayemkataa Yesu

Kristo katika siku za mwili Wake duniani. Yesu alisema jambo hilo, “Ukisema neno juu ya Mwana wa Adamu,” wakati wao waliposema ya kwamba alikuwa mpiga ramli ama pepo fulani mchafu, kasema, “ukisema neno juu ya Mwana wa Adamu, utasamehewa. Lakini yeye anayesema Neno juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa kamwe katika ulimwengu huu,” hiyo ni kusema, kuita kutenda kazi kwa Roho Mtakatifu kwamba ni jambo ovu, chafu, wakati wanaona kazi ya Mungu ikifanyika.

⁴⁵ Naam, Yona alikuwa shahidi wa ufufuo, kwa kuwa alikuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku. Watu wengi wanakazana kumhukumu Yona, na kusema ya kwamba, “Loo, yeye, kila mtu, yeye alikuwa Yona fulani.” Yona alikuwa nabii. Yeye alikuwa akienda kabisa katika mapenzi ya Mungu. Wakati alipopanda ile merikebu nyingine na kuelekea huko, hilo lilipaswa kutendeka, haina budi kuwa hivyo ili kuonyesha kufufuka kwa Yesu Kristo. Ilimbidi atimize sehemu hiyo, kama tu vile Hajiri alivyofukuzwa, ili kwamba yule mwanamke huru asirithi na kijakazi. Mambo haya yalipaswa kutukia, yalikuwa ni vivuli na mifano ya mambo yajayo.

⁴⁶ Sasa tunaona, Yeye anashuka basi, baada ya kunena juu ya Yona, Naye anakuja kwenye wakati wa Sulemani. Sasa, sote tunajua ya kwamba wakati wa Sulemani ulikuwa ni ule Utawala wa Miaka Eflu, karibu, wa Agano la Kale. Ulikuwa ndio wakati uliokuwa mkuu sana, wa zote Israeli walizowahi kupata, ulikuwa ni chini ya utawala wa Sulemani; hakuna kuzungumzia habari za vita, na walikuwa na wakati wa raha sana. Mungu alimpa Sulemani, ambaye alikuwa Mwana wa Daudi, alimpa karama ya upambanuzi, na sasa yeye angeweza kutambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa watu.

⁴⁷ Sasa, vipi ambavyo huyo Mwebrania aliyekuwa akisimama pale alipaswa kutambua jambo hilo! Sulemani alikuwa—alikuwa na karama ya upambanuzi naye aliweza kuyatambua mawazo ya mioyo yao, nao wote wakamfuata Sulemani, na hata hivyo hapa alisimama aliye mkuu kuliko Sulemani. Naye Sulemani alikuwa Mwana wa Daudi, lakini yeye alikuwa mwana mdogo wa Daudi, kimwili; naye Yesu alikuwa Mwana wa Daudi, kwa Uzao wa ahadi, Mzao wa kifalme. Na hapa alikuwepo aliye mkuu kuliko Sulemani amesimama pale, akifanya jambo lile lile alilofanya Sulemani, ila tu alikuwa mkuu kuliko Sulemani, nao wakaita jambo hilo “Beelzebuli.”

⁴⁸ Mnaona kufasiriwa kwa Maandiko? Si ajabu Yeye alisema yale aliyosema, “Kizazi kichafu na cha zinaa kitatafuta ishara; nao wataipata, ishara ya kufufuka.”

⁴⁹ Na katika wakati wa Sulemani, kulikuweko na ufufuo mkuu unaendelea. Kwa namna fulani nitalielezea kwa mfano, ili vijana wapate kulielewa. Kulikuweko na ufufuo mkuu uliokuwa unaendelea katika siku za Sulemani. Mungu alitoa karama, na

taifa zima likaifuata hiyo. Kila mtu alijia. Waliiamini, kwa moyo wao wote.

⁵⁰ Je! hilo si lingekuwa ni jambo zuri sana kama lingetukia miongoni mwa watu usiku wa leo, kama Marekani yote, watu wote wanaojiita Wakristo, wangeifuata karama ya Mungu katika siku hizi za mwisho, kule kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya watu! Hiyo ndiyo karama ya Mungu katika siku hii ya mwisho, ni Roho Mtakatifu. Kristo, katika mfano wa Roho, Yeye yuko hapa pamoja nasi sasa. Si lingekuwa jambo zuri sana kama makanisa yote yanayokiri kuwa Wakristo, yangeifuata karama hii kuu ambayo Mungu ametupa sisi?

⁵¹ Ni kwa nini? Wao wametoka wakaenda kwenye kila namna za itikadi na kanuni za imani na mafundisho ya sharti, na huwezi kusema nini ni nini. Ni vile vile kabisa walivyotenda daima. Lakini Mungu aliahidi kwamba jambo hilo litatatuliwa, kwa ule Mzao, hata hivyo, wakati wa mwisho.

⁵² Sasa angalia katika jambo hili, tunaona ya kwamba hao wote waliunga mkono karama ile kubwa, na Israeli wakafanikiwa sana kuliko walivyowahi kufanikiwa. Mataifa yote yaliiogopa Israeli; waliogopa kuja kule, kwa maana walijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja nao.

⁵³ Nami nawaambia, mnazungumza juu ya kuukomesha ukomunisti na kila kitu; hebu Marekani na imrudie tu Mungu, iirudie karama yake, imrudie Roho Mtakatifu, na watu wataacha kupigia makelele ukomunisti. Huo umeoza sana hivi kwamba hata wakomunisti wana makachero wa kuupinga ukomunisti, kupeleleza wajue wao ni akina nani. Jambo hilo halina budi kuwa namna hiyo. Lakini hebu na warudi!

⁵⁴ Hapa si muda mrefu uliopita, huko Finland. Ndugu Lindsay, ninaamini, yeye—yeye alikuwa hapa jana usiku, alikuwa pamoja nami wakati jambo hilo lilipotukia. Mvulana mdogo, ambaye nilikuwa nimemwona kwenye ono hapa, alifufuliwa katika wafu, hapa. Wengi wenu, nadhani, mngali mmeliandika katika Biblia zenu, nilipokuwa ninaenda kila mahali nchini, nikisema vile angeonekana, mahali ambapo angekuwa, na kadhalika. Naye alifufuliwa kutoka kwa wafu, kulingana na Neno la Bwana. Alikuwa ameuawa katika ajali ya barabarani. Wengi wenu mnakumbuka kisa hicho, na nilisimama pale wakati alipofufuka katika wafu.

⁵⁵ Usiku huo, nikishuka kwenda Messuhalli. Mimi pamoja na Ndugu Lindsay, na Ndugu Moore, na wengi wa watu hao, wakifanya bidii kushuka kwenda Messuhalli; ambako, waliwaachilia maelfu wengi, wakaniruhusu kuzungumza nao, kisha wanaondolewa halafu ninazungumza na wengine. Tulipokuwa tukishuka kwenda kule, walikuwa wamefunga barabara urefu wa majengo manne ama matano ya mji. Watu walikuwa ba—barabarani, kutuangualia tukiingia na kutoka. Na

mle ndani, kulikuweko na msichana mdogo ambaye alikuwa na mikongojo, mguu mmoja ukiwa mfupi kuliko huo mwingine, alikuwa ameponywa, na mambo mengi yalikuwa yamefanywa.

⁵⁶ Halafu mvuluna huyu mdogo alipofufuliwa, ikatangazwa kwenye taarifa ya habari. Hao hawana rumba na upuuzi, huko Ufini, ama hawakuwa na hayo wakati huo. Kulikuweko tu na matangazo ya habari na mambo yaliyo muhimu, ndiyo waliyokuwa nayo redioni. Na habari hizo zilikuwa zimeenea kila mahali mpaka zikafika Urusi. Kama unaishi Urusi, na maili arobaini kutoka nyumbani kwako, mahali ulipozaliwa, huna budi kupata visa kuonyesha shughuli zako. Na zile. . . zile nchi za Pazia la Chuma zilikuwa moja kwa moja. . . tulitembea moja kwa moja tukaingia kule, ambako bomu-bomu zilikuwa zimewekwa barabarani, nje tu ya Kuopio. Na usiku huo, habari hii ilikuwa imetangazwa, na barabara zilikuwa zimejaa maelfu mara elfu ya Warusi.

⁵⁷ Hapa kulikuwa na wale wanajeshi wa kikomunisti, wanajeshi wa Kirusi, wamevaa hizo kofia ndogo za duara; na wavulana wadogo sita wa Kifini, mara baada ya vile vita, hawakuwa na umri wa kutosha kukata ndevu, walikuwa wavulana wenye nyuso laini; wamevaa mabuti makubwa machakavu, makoti makubwa marefu, wakitembea barabarani, wakiwa na hivi vitara na kadhalika, wakinilinda nipate kupita kwenye umati niweze kuingia. Hapa walisimama hao Warusi wakisimama pale. Nilipopitia pale, walinipa gwaride la heshima, wakasimama namna *hii*, huku majonzi yanatiririka mashavuni mwao. Na wakati nilipopitia pale, wao waliwakumbatia wale wanajeshi wa Kifini na kuwapigapiga mgongoni, na kuwakumbatia. Kitu cho chote ambacho kingemfanya Mrusi kumpigapiga Mfini kwa upendo, kitakomesha vita. Wakasema, “Huyu tutampokea, Mungu ambaye anaweza kuwafufua wafu.”

⁵⁸ Hiyo ndiyo shida usiku wa leo, ewe rafiki, kweli. Kilichowafanya kuwa wakomunisiti, ni kwa sababu makasisi wameliacha Neno la Mungu. Wamechukua fedha zote, na hawana kitu cha kuwapa badala yake, ni kama tu loji ama cho chote kile. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu.

⁵⁹ Ndipo tunaona ya kwamba katika siku za Sulemani, wote walikuwa wakiiunga mkono karama hii kuu ambayo Sulemani aliipata kutoka kwa Bwana. Nao watu walikuwa wakija na kwenda. Mataifa yote yaliwaogopa Israeli. Badala ya kujaribu kufanya vita nao, walileta matoleo ya amani. Hawakumwogopa, sana, mtu wao, walimwogopa yule Mungu waliyekuwa wana umoja Naye.

⁶⁰ Loo, hilo lingekuwa jambo la namna gani kwa taifa hili, usiku wa leo, kama sote tungekuwa tunamcha Mungu, kama sote tungalimheshimu Mungu, na kupokea kipawa Chake cha

Roho Mtakatifu na kumfuata, kila kanisa livunje kanuni zao za imani na kuzitupilia nje, na kwenda madhabahuni na kukaa pale mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja kulitambulisha Neno Lake katika siku ya mwisho!

⁶¹ Wengine wao wakijaribu kusema, “Mbona, Hiyo ni kwa ajili ya Wayahudi peke yao kuipokea. Hapakuweco na la zaidi.”

⁶² Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, na makabatizwe kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjje.” Mradi tu kuna Uzao unaongojea duniani, kuitwa, kuna Roho Mtakatifu wa kuuita Kwake. Hiyo ni kweli. Lingali ni jambo lile lile tu.

⁶³ Lakini tunaona, anapokuja, anakataliwa. Hiyo ndiyo sababu taifa linakuwa chini ya laana. Hiyo ndiyo sababu mambo yanaendelea jinsi yanavyoendelea usiku wa leo.

⁶⁴ Na tunaona katika wakati wa Sulemani, haikuwa hivyo. Wote waliifuata karama hiyo ya upambanuzi ambayo Sulemani alikuwa nayo. Nayo mataifa yote yakamcha Mungu. Na habari zikaenea kila mahali, “Loo, laiti ungalikuja Israeli, Mungu wao ameinua karama miongoni mwao nao wamemfanya mfalme. Na hekima yake, upambanuzi wake, umepita akili ya mwanadamu. Umepita. ‘Uko kwenye ulimwengu wa miungu ndani huko kabisa,’ ndiyo makafiri wangesema. Nasi hatufahamu jinsi ilivyo, lakini Mungu, Mungu wao, amejiwakilisha Mwenyewe katika mmoja wa waamini wao. Na, yeye, wamemweka kwenye kiti cha enzi, nao wote wanamsikiliza.” Mnajua, habari wakati huo hazikuenezwa kwa televisheni, simu, na kadhalika, ilikuwa mdomo kwa sikio.

⁶⁵ Hatimaye habari zikaenea moja kwa moja huko chini kupita Jangwa la Sahara, zikaenea mpaka zikafika katika nchi ndogo iliyoitwa Sheba. Walikuwa na ninii . . . Ilikuwa nchi ya makafiri. Walikuwa na maskini malkia mmoja kule, hapana shaka alikuwa mwanamke m—mzuri wa kuheshimika. Basi habari zikamfikia, ya kwamba, “Mungu alikuwa anatoa ufufuo mkubwa kule katika nchi ya Israeli, na mambo makuu yalikuwa yakitukia. Nao walikuwa na mtu huko aliyetiwa mafuta na Roho wa Mungu wao, ya kwamba huko hekima yake ilipita kitu cho chote ambacho mwanadamu angeweza kuwazia.”

⁶⁶ Mwajua, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

⁶⁷ Jambo hilo lilichochea maskini moyo wake. Akaanza kuwazia juu ya jambo hilo. Na sasa, wakati kila msafara ulipokuwa ukipita, hapana shaka, maskini malkia huyo angewatuma wanajeshi wake, na kusema, “Ningetaka kuzungumza na mtu huyo, faraghani, kama ametoka Israeli.”

68 “Naam, malkia, tumekuwa huko Israeli, na, loo, ni ajabu sana. Unapaswa kuona jambo hilo. Hakuna kitu kinachofanana na jambo hilo. Kimepita ufahamu wa mwanadamu. Unajua, wote wako katika nia moja, kila mmoja wao anaifuata karama hiyo vizuri ambayo Mungu wao amewapa, na wote wanaiamini kwa moyo mmoja. Loo, ndilo jambo la fahari sana, wala hakuna jambo lo lote lililofichwa. Mungu hufunua tu kila kitu. Kama taifa lo lote lingeanza kuwaingilia kule, mbona, huyo Mungu wao angefunua mahali walipokuwa wanapitia, na—nao wawavizie kabla hawajawafikia kule. Loo, ulikuwa tu ni ufufuo mkubwa ukiendelea.”

69 Halafu, unajua, maskini malkia huyo anaanza kuona njaa ya kuona jambo hilo, yeye mwenyewe.

70 Unajua, kuna jambo fulani juu ya jambo hilo, mwanadamu anajua anatoka mahali fulani; naye yuko hapa, yeye hajui ni kwa nini yuko hapa; naye anaelekea mahali fulani, wala hajui anakoenda. Na kuna Kitabu kimoja tu ulimwenguni kinachotwambia sisi ni nani, mahali unakotoka, wewe ni nini, na mahali unapoenda, nacho ni Biblia. Ndicho pekee kinachokwambia, nacho ni Kitabu cha Mungu. Ni Mungu Mwenyewe aliyedhihirishwa katika umbo la neno, linaloitwa Mbegu. Mbegu hiyo ikipandwa katika ardhi nzuri itazaa kila ahadi aliyoahidi Yeye, maana ni Mungu Mwenyewe. Lakini haina budi kunyweshewa maji kwa imani, kuifanya itimie, kama mbegu nyingine yo yote. Chembe ya uhai imo ndani yake. Twajua. Angalia sasa.

71 Tunaona ya kwamba katika kufanya jambo hili, maskini malkia huyo akaanza kuona njaa na kiu ya Mungu. Loo, laiti—laiti karama za Mungu zingaliweza tu kuumba kiu katika moyo wa watu, kwa ajili Yake, kama ilivyomfanyia yule mwanamke!

72 Sasa tunaona, ili kwamba watoto, hao jamaa wadogo, kuna safu nzima yao walioketi hapa na mahali pengine, ili wapate kufahamu, tutalielezea kwa namna fulani ya mchezo wa kuigiza kwa ajili yao, ili kwamba wapate kufahamu.

73 Sasa kumbukeni, yeye alikuwa mpagani. Kwa hiyo ili alifanye jambo hili, na akiwa ni malkia, ingembidi kupata ruhusa kutoka kwa kuhani wake wa kipagani, kusudi apate kwenda. Nami ninaweza kuwazia nikimwona huyo malkia akienda kwa kuhani na kuinama, na kusema, “Baba mtakatifu mkuu *fulani*, tunajua ya kwamba Israeli wana ufufuo huko, na Mungu wao amejiwakilisha katika umbo la mwanadamu, kwa karama kuu, hivi kwamba anajua siri za moyo. Nao wananiambia ya kwamba Yeye ni Neno, nalo Neno huyatambua mawazo ya moyo, nao wanasema ya kwamba inafanya kazi ndani ya mtu. Ningetaka ruhusa yako, ewe baba uliye mtakatifu sana, ya kupanda kwenda huko, nikazuru nijionee mwenyewe.”

⁷⁴ Vema, ninaweza kuwazia jibu lake likija. “Sisi hatuna ushirikiano wo wote katika ufufuo huo,” ama hiyo ni picha ya ‘64 ya jambo hilo. Lakini, hata hivyo, wao—wao wanasema, “Si wafuasi wa madhehebu yetu. Wao si wa watu wetu. Hatuna uhusiano wo wote na kitu hicho, hata kidogo. Hutaenda. Nao si kitu cho chote ila ni kundi la—la wenda wazimu. Wanasikiliza kila namna ya uvumi kuhusu wao juu yao kupitia katika Bahari fulani ya Shamu, na kila upuuzi wote wa namna hiyo, lakini hakuna kitu cho chote kuhusu jambo hilo. Huyu *hapa* mungu wetu aliye mkuu, unamwona amesimama ukutani? Walikuwa *kadha-na-kadha* na mara nyingi sana wamefanya *kadha-na-kadha*.” Maskini malkia huyu akaondoka amechukizwa sana.

⁷⁵ Lakini, mnajua, kuna jambo fulani juu yake, kama Mungu akianza kuweka njaa ndani ya moyo wa mwanadamu, hakika hakuna kitu kitakachouzia. Kama kuna ushirikiano ama hakuna, ama kama kuna jambo lo lote, hana budi akipate kitu Hicho! Kama nilivyosema kuhusu maskini yule mwanamke jana usiku, akiwa ameshikilia na kung’ang’ania. Unaona, kitu Fulani kinakushikilia, nawe unashikilia kitu Fulani. Kama vile Yakobo, mwana wa—wa Mungu; Yakobo, mwana wa Mungu, alivyoshikilia kitu Fulani usiku mmoja, Nacho kikamshikilia; naye kamwe hakukiachilia mpaka alipopata alichotaka, akabarikiwa Nacho. Hilo, hilo ndilo jambo halisi. Na wakati mtu aigizapo kitu fulani, kamwe hakijawahi kufanikiwa. Lakini kama tu unaweza kushikilia kitu Fulani, na kitu Fulani hicho kinakushikilia, litatukia.

⁷⁶ Kama ukija hapa usiku wa leo kwa ajili ya uponyaji, na umwache Roho Mtakatifu akushikilie, nawe umshikilie Yeye, utapata kile unachoomba. Hakuna njia ya kukutenganisha Nacho.

⁷⁷ Ukija ukiamini ya kwamba Yesu Kristo huokoa, na kuna nguvu ya kuokoa inakushikilia, nawe unaishikilia Hiyo, utaokoka.

⁷⁸ Kama unaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu anakushikilia, Naye atakubatiza, nawe umshike Yeye; haitakulazimu kuondoka kwenye kiti chako, Yeye atakujaza na Uwepo Wake papo hapo ulipo. Kama tu alivyokwisha fanya Yeye, “Petro alipokuwa angali akinena maneno haya, Roho mtakatifu akawashukia hao waliolisikia.” Kitu Fulani kilishikilia!

⁷⁹ Kitu Fulani kilimshika maskini yule mwanamke Msirofoinike tuliyenena habari zake jana usiku. Haidhuru alipata vipingamizi vingapi, yeye angali alikuwa anaendelea, hata hivyo. Kitu Fulani kilimshika maskini huyu malkia tunayenena habari zake usiku wa leo, mpagani, kafiri. Vivyo hivyo huyu mwanamke Msirofoinike, Myunani, mpagani,

mwabudu sanamu. Lakini kitu Fulani kiliwashikilia, nao wakashikilia kitu Fulani.

⁸⁰ Daima kuna magumu njiani. Shetani hutupa kila kitu njiani, awezacho, wakati anapoona kitu halisi cha Mungu kimeanzishwa. Atakufanyia jambo hilo. Ataweka kila kitu, vipingamizi vyote awezavyo, njiani mwako.

⁸¹ Kumbuka, huyo mwanamke alikuwa na vipingamizi vingi sana, lakini imani yake haikuwa na vyo vyote. Imani haina kipingamizi. Hakuna kitu kitakachoisimamisha, hata mtu ye yote aseme nini. Kama umemshikilia Mungu vizuri, Mungu anakushikilia vizuri; kunaweza kuwe na madaktari arobaini wamesimama hapa wakikwambia wewe unakufa, nawe hungeamini hata neno moja lake. La, bwana. La, bwana. Kungeweza kuweko na makasisi arobaini wamesimama hapa, kama wale mia nne wa Ahabu, kukabilia na we; kama wewe ni Mikaya nawe umemshikilia Mungu, Mungu amekushikilia, na unaliona limethibitishwa katika Neno, hakuna kitu kitakachokuzuia. Utasimama pale, kwa vyo vyote, kwa sababu kitu Fulani kimekushikilia.

⁸² Ilifunuliwa kwa maskini mwanamke yule, ya kwamba kulikuweko na Mungu mahali fulani. Ninaweza kumwona akienda na kusoma hayo magombo ya Kiebrania tena, anayafingirisha na kuyaweka katika—katika mtungi; na kurudi kwa yule kasisi wa kipagani, na kusema, “Ninataka kukwambia jambo fulani, baba mtakatifu. Huenda ikawa ni kweli, mambo hayo unayosema. Lakini, angalia, nyanya yangu aliabudu sanamu hiyo, alisoma katekismo hiyo uliyo nayo. Mama ya nyanya yangu aliisoma, na mama yangu aliisoma, watu wangu wote waliisoma, yote ni juu ya jambo fulani lililotukia. Sijapata kuiona ikisogea, bado. Lakini wao wananiambia wana kitu Fulani huko juu ambacho ni halisi, kinatenda kazi sasa hivi; si historia fulani, lakini kitu fulani kinachoendelea sasa.”

⁸³ “Sasa angalia hapa,” yeye angesema, “mtoto wangu. Kama ukienda, nitakutoa ushirikani. Nawe huna shughuli yo yote, kama malkia, kujihusisha mwenyewe na watu kama hao.” Ibilisi yuyo huyo wa kale angali anaishi.

⁸⁴ Hakuna kundi lililo bora zaidi ulimwenguni, kujiunga nalo, kuliko kanisa lililozaliwa mara ya pili lililozajwa Roho Mtakatifu. Sijali liko wapi, kama liko kwenye vichochoro vya mji ama po pote lilipo. Ndilo kundi bora kuliko yote. Ni kundi la kimbinguni, angalia, waamini wanaomwamini Mungu.

⁸⁵ Moyo wake ulikuwa unadundadunda sana, kwa matarajio. Yeye alitaka kuona. Alikuwa amesikia habari zake. Hakujuu cho chote kuhusu jambo hilo, lakini alitaka kuliona. Nami ninaweza kumsikia akisema, “Vema, unaweza tu kuliiondoa jina langu kwenye kitabu, kama ukitaka. Lo lote usemalo, na hizo sanamu, na hivyo vitabu na kadhalika, ninaona ukiendelea kuniambia

juu ya jambo fulani, ukisema juu ya jambo fulani. Hakijasogea kamwe. Sijapata kuona msogeo mmoja wake bado. Ninataka kitu fulani ambacho ni halisi,” naye anajiandaa kwa safari. Inasikitisha sana hatuna maskini malkia wengi zaidi kama hao siku hizi! Hakika.

⁸⁶ Kwa hiyo basi tunaona ya kwamba sasa, kusudi apate kuondoka, alitumia mbinu nzuri sana. Ningetaka kila mtu awazie jambo hili. Sasa Yeye alisema hakujua. Alikuwa amesoma magombo yote, apate kujua Yehova alikuwa ni nini, kuona jinsi alivyokuwa amefanya kazi katika siku zilizopita. “Kama hiyo ni kweli, basi Yeye angejitambulisha kwa mtu huyu kama vile watu walivyosema mtu huyo alikuwa, basi alikuwa Yehova. Na kama ilikuwa ni Yehova, Naye alikuwa ni Mungu wa kweli, Mungu wa walio hai, si sanamu fulani ama mnara wa kiumbe fulani kilichoishi zamani ama hakikuishi; huyu alikuwa Mungu aliye hai, aliyepo sasa hivi,” kwa hiyo alitaka kujitayarisha kwenda. Sasa akasema . . .

⁸⁷ Alipakia pesa nyingi sana. Alichukua dhahabu, manemane na, loo, ubani, nadhani, na fedha. Naye alikuwa amesheheneza ngamia kwa mali hiyo. Sasa yeye akasema hivi, “Ninatapanda niende. Nitaenda niliangalie, mimi mwenyewe. Na basi kama ndivyo ilivyo, nitaliunga mkono; kama si la kweli, sitajihusisha nalo kwa vyo vyote.”

⁸⁸ Unajua, angeweza kuwafundisha Wapentekoste jambo fulani. Wengi wao husaidia miradi ambayo inawacheka na kuwadhihaki. Halafu mnasaidia kipindi cha redio, kinachofanyia mzaha mambo ambayo mnaamini. Na hiyo ni kweli. Naam, bwana. Kwa sababu kinaonekana kwamba ni cha kweli. Hakika, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu,” Yesu alisema.

⁸⁹ Lakini mwangalie yeye, yeye alisema, “Kama sivyo ilivyo, basi ninaweza kurudisha zawadi zangu.” Lakini alikuwa akienda kujionea mwenyewe, na ashawishike. Alikuwa amesoma yale magombo, alijua Yehova alikuwa ni nini, naye angeona. Kama alikuwapo, Yuko leo, basi Yeye angali ni Yehova.

⁹⁰ Hilo ni jambo zuri leo. Yesu Kristo yuko vile alivyokuwa, na daima atakuwa hivyo. Yeye habadiliki kamwe. Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁹¹ Tunamwona maskini mwanamke huyo basi, nena kuhusu vipingamizi, basi jambo hili huenda lilingia mawazoni mwake, “Kumbukeni, sina budi kuvuka jangwa, na hiyo ni safari ndefu sana.” Ipime, kutoka Israeli, kutoka Palestina ushuke ufike huko Sheba, kuvuka Jangwa la Sahara. Ingemchukua ngamia kama, nafikiri, huo msafara, iliwachukua siku tisini, miezi mitatu, wakisafiri wakati wote, kutoka mahali pamoja mpaka mahali pengine. Siku tatu . . . miezi mitatu, kwenda. Na hebu wazia tu, alivuka hilo jangwa lenye joto. Yeye alikuwa na jambo hilo

moyoni mwake, ilimbidi kufanya jambo hilo, kuvuka hilo jangwa lenye joto, umbali wote kufikia kule, apate kujua kama huyu kweli alikuwa ni Mungu.

⁹² Si ajabu Yesu alisema, “Yeye atasimama pamoja na kizazi hiki na kukihukumu.” Hakuwa na Kadilaki yenye kubaridisha. Na watu wengine hapa Dallas hawatavuka barabara, kulisikia. Hiyo ni kweli. Si ajabu atasimama katika siku za mwisho! Lakini kusimama mahali fulani na kulilaumu, mahali pengine po pote wanalilaumu. Kasema, “Yeye alitoka katika pande za mwisho za dunia kusikia hekima ya Sulemani, na aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Angalia.

⁹³ Ilimbidi kukabiliiana na hayo. Labda ilimbidi kusafiri usiku, ni joto sana jangwani. Mionzi ya moja kwa moja ya jua juu ya hilo Jangwa la Sahara ingekuchuna ngozi, na pale ilimbidi labda kusafiri usiku.

⁹⁴ Jambo lingine, kumbuka, alikuwa amelemewa na mizigo ya zawadi na kadhalika. Wana wa Ishmaeli walikuwa wapanda farasi hodari sana. Walikuwa wanyang’anyi wa jangwani. Ingekuwa rahisi jinsi gani kwa wana wa Ishmaeli kuwavamia kama gharika, na kuwakatilia mbali maskini hao matowashi wawili ama watatu aliokuwa pamoja nao; hilo kundi lake dogo la askari, matowashi, na maskini wajakazi wake; wawakatilie mbali na kuwaacha wamelala pale, na kunyakua johari zenye thamani ya maelfu kumi mara maelfu ya dola, mbali na ubani na manemane vilivyo na bei ya juu sana, na vitu alivyokuwa anavileta kama zawadi.

⁹⁵ Lakini kuna jambo fulani katika jambo hilo, kama moyo wako umeelekezwa kumwona Mungu, na kitu Fulani kimekushikilia, hujui hatari yo yote, hujui kushindwa. Kuna jambo fulani, utalipata, hata hivyo, hata kuwe na shida gani.

⁹⁶ Hakika, ilionekana kama ni biashara nzuri sana kwa wanyang’anyi. Ye yote wao angaliweza kuja, lakini yeye hakufikiria juu ya hatari yo yote.

⁹⁷ Yeye hakuwazia kama angaliweza kuamka na kutembea, kama mtu anayeogopa kuamka kitandani ama kitanda cha mtoto mdogo, ama cho chote kile, “Sijui mimi, unaona, ninaogopa kufanya jambo hilo.” Yeye hakuwa na woga wa namna hiyo. Kitu Fulani kilikuwa kimemshikilia.

⁹⁸ Na kama kitu Fulani kinaweza kutushikilia, kwa jinsi hiyo hiyo, jambo fulani litatukia. Sasa, huwezi kufanya jambo hilo mpaka Hicho kikushikilie, afadhali usithubutu. Lakini wakati Hicho kimekushikilia, litatukia.

⁹⁹ Angalia, huyu hapa, yeye hakuambiwa kamwe kwamba ni wanyang’anyi wangapi waliokuwa huko jangwani.

¹⁰⁰ Ama, tena, alipofika kule, je! atapokelewa, ama hatapokelewa? Yeye alikuwa wa madhehebu mengine, mwajua,

kwa hiyo je! yeye angapokelewa, je! angepokelewa mkutanoni? Yeye hakuombwa aje. Roho Mtakatifu alitenda kazi ndani yake, kusudi aje, kwa hiyo Yeye alikuwa ndiye aliyekuwa anaongoza; ili kwamba, apate kuridhisha kujihisi kule alikokuwa nako, ambapo alitaka sana kujua.

¹⁰¹ Kumbuka, *maisha* ni yako. Ilikuwa ni maisha yake. Una wakati mmoja tu wa kutatua jambo hilo, na huenda ikawa usiku wa leo ndiyo nafasi yako ya mwisho. Ukimkataa Kristo, usiku wa leo, huenda usiwe na nafasi nyingine.

¹⁰² Na hiyo huenda ilikuwa ndiyo nafasi yake ya mwisho. Yeye alitambua jambo hilo. Je! hiyo dini yake baridi, ya kawaida, aliyokuwa nayo, ilikuwa sawa, ama kulikuwako kweli na Mungu aliye hai? Hakuwa ameona kitu katika dini yake mwenyewe, lakini alikuwa amesikia kulikuwako na kitu Fulani katika ile nyingine, naye alikuwa amesoma yale Yeye aliyokuwa. Alitaka kuona. Maisha yake ndiyo yaliyokuwa hatarini.

¹⁰³ Ni maisha yangu, usiku wa leo, sina budi kukabiliana na jambo hili. Sina budi kuja Hukumuni, vivyo hivyo nawe pia huna budi kuja Hukumuni. Inatupasa kuketi vitini mwetu, tulale vitandani mwetu, ama po pote tulipo, na kutafakari mambo haya kindani. Kwa sababu, hujui ni wakati gani kadi yako itakapotolewa kwenye rafu ya Mungu Kule juu, nawe utatoa hesabu Hukumuni. Kama wewe ni mfuasi wa kanisa ama la, hilo halina uhusiano wo wote nalo. Utawajibika, hata hivyo, na afadhali uwe na hakika kabisa juu ya jambo hilo. Chunguza ujuzi wako na Mungu, angalia kama Kitu Fulani kweli kimekushikilia, kinachokurudisha kwenye Neno hili, mbali na kanuni za imani na taratibu, na kadhalika. Yeye aliahidi jambo hilo katika siku za mwisho, “Kungekuwako na kugeuzwa, tena, kwa mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.” Nasi tunaamini jambo hilo. Angalia, tunaona jambo hilo katika siku hii sasa.

¹⁰⁴ Wala hakuwazia juu ya woga ama cho chote kile kitamsumbua. Hakuwa akiwazia jambo hilo. Wazo hilo lilikuwa, alitaka kujua kama jambo hilo lilikuwa ni halisi ama si halisi, kwa hiyo moja kwa moja akaenda zake kuvuka jangwa. Wala si nini. . . Alikuwa na wakati mgumu kulitenda hilo. Lo lote ambalo unaninii. . .

¹⁰⁵ Shida ndiyo hiyo, Sisi Wapentekoste, tunapewa kila kitu, kwenye chano, kila kitu tunachotaka. Kama mchungaji asipowahi kuja mapema, “Nitaliacha Assemblies nikajiunge na kanisa la Mungu.” Na, unajua, ni ninii tu. . . tunabembelezwa sana kila mahali!

¹⁰⁶ Inanikumbusha mimi, kulikuwako na baharia mzee, wakati mmoja, akitokea baharini. Na mshairi mmoj alishuka kwenda kule, hajawahi kuona bahari; alikuwa ameandika habari zake,

lakini hajawahi kuiona. Baharia yule mzee akakutana naye, akasema, “Unaenda wapi, rafiki yangu?”

¹⁰⁷ Akasema, “Ninaenda baharini. Mimi ni mshairi. Nimeandika juu ya bahari. Nimetamani sana kusikia harufu ya bahari, na nione mawimbi yake makubwa ya gharika yakiruka kuwazunguka shakwe wanaoimba, na anga la samawati likijiakisi baharini.”

¹⁰⁸ Huyo baharia mzee akapulizia kiko chake mara nne ama tano, akaangalia chini, na kutema mate. Akasema, “Nilizaliwa humo, miaka sabini iliyopita. Sioni kitu cho chote kinachovutia sana kwake.” Yeye alikuwa ameishi humo, kwa muda mrefu sana, mpaka kikawa ni kitu cha kawaida.

¹⁰⁹ Hivyo ndivyo ilivyo kwetu, usiku wa leo. Tumeishi katika Uwepo wa Mungu, muda mrefu sana, mpaka imekuwa ni kitu cha kawaida kwetu. Tunapaswa kuamka, na kutambua ya kwamba Yesu Kristo yu hai na amefufuka katika wafu.

¹¹⁰ Hili lingekuwa ni tukio jipya kabisa kwa maskini malkia huyu. Yeye alikuwa anang’ang’ana. Alitaka kuona hilo. Kwa kweli, alikuwa thabiti. Ilibidi awe thabiti, kuondoka nchini mwake. Ilibidi heshima zake zote, ilibidi kuziacha nyuma. Vipi kikundi chake cha karata na vikundi vyote alivyokuwa memba wake, vikundi vyote vya kushona na ushoni, na yote aliyokuwa mshirika wake, kama malkia, watu wote maarufu aliowajua? Yeye angekuwa mtu wa kuchekwa kwa kundi hilo. Lakini hilo lilileta tofauti gani kwake? Swala lilikuwa ni nafsi yake.

¹¹¹ Ni nafsi yako. Ni nafsi yangu. Inaleta tofauti gani kwa Mmethodisti, Mbatisti, Presbiteri, ama wa Umoja, Uwili, Utatu, ama yo yote yale? Nafsi yangu ndiyo inayohusika. Nafsi yako ndiyo inayohusika. Neno la Mungu ndilo linalohibitishwa.

¹¹² Tunamwona yeye, haikuleta tofauti yo yote kwake, yale mtu ye yote aliyosema, ama yale watu wake mashuhuri, yale rafiki zake, iwapo ilimbidi kuacha kila kitu kilichokuweco ulimwenguni. Kama lilikuwa ni jambo halisi, yeye alikuwa tayari kuliendea jambo hilo. Angetoa ufalme wake, cho chote kile. Kama lilikuwa ni jambo halisi, yeye alitaka kumpata Mungu. Kulikuweco na jambo fulani moyoni mwake.

¹¹³ Tunaona, huyu hapa anavuka lile jangwa. Hatimaye, siku baada ya siku, siku tisini, miezi mitatu, huo msafara hatimaye ukawasili langoni.

¹¹⁴ Sasa, yeye hakuja kama vile watu wengi wanavyofanya kwenye mikutano siku hizi. Wengi wao wanakuja na watasema, “A-ha, ninasikia wananinii, a-ha, mtu fulani aliniambia ya kwamba walikuwa na...A-ha. Vema, nitaenda kule.” Nao wataketi kwa dakika chache tu. Waangalie. Unawaona kila mahali. Watasema, “Neno la kwanza atakalosema ambalo ni kinyume cha imani yangu,” wanatoka nje, wanaenda zao.

“Sitarudi kule kusikiliza lingine tena.” Unaona, wao hawaketi muda mrefu wa kutosha. Naam.

115 Vipi kuhusu wakati, Yesu, wakati alipokuwa ameketi mbele ya wale watu wake sabini pale, Naye alikuwa na wale sabini na alikuwa na umati wote? Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri. “Alikuwa Nabii,” walisema, “yule Nabii wa Galilaya.” Siku moja aliangalia umati huo mkubwa uliomzunguka, akasema, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.”

116 Ungeweza kuwazia madaktari walioketi huko, waliyosema kuhusu Mtu huyo? “Mbona, atatufanya sisi vizuu vifyonza damu. Ati tuinywe Damu Yake na kuula mwili Wake?”

117 Yeye kamwe hakueleza jambo hilo. Haikumbidi kulieleza. Ilimbidi kuvitikisa vile vimelea vilivyomzunguka vianguke. Badala ya kujaribu kuwabembeleza na kuandika jina lao kwenye kitabu fulani, Yeye alikuwa anawatikisa waanguke. Hakutaka kuwatumia tena. Kwa hiyo tunamwona, Huyu hapo, akasema, “Msipoula . . .” Hakueleza jambo hilo kamwe.

118 Angalia, hao wanafunzi waliketi kimya. Hawakusema neno.

119 Nawaona madaktari na Mafarisayo, kasema, “Mnaona, Mtu huyu amerukwa na akili. Ni kichaa, ati anataka tuukate mwili Wake sasa na kuula, kisha tunywe Damu Yake? Kizuu cha binadamu! Vema, sisi, hatungeweza kufanya jambo kama hilo. Loo, hicho ni kichaa. Mtu huyo amerukwa na akili.” Wakaondoka.

120 Ndipo akawaangalia hao wanatheolojia waliokuwa wamemzunguka, hao sabini, akasema, “Mtasemaje mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa Mbinguni alikotoka?” Hao Madaktari wa Uungu wakiangalia kila mahali, wakasema, “Ati Mwana wa Adamu apae Mbinguni alikotoka? Mbona, sisi tunamjua Yeye, tumefika kwenye hori alikojaliwa. Tumeona kitanda alimolazwa. Tunamjua mama yake. Sisi . . . Anavua samaki pamoja nasi. Anawinda pamoja nasi. Yeye anarandaranda huko milimani. Anavaa nguo tunazovaa, anakula chakula. Na huyu Mwana wa Adamu, alitoka wapi? Alitoka Nazareti. Hili linatushida sisi.” Hao wakaenda zao. Bado hakueleza jambo Hilo. Mnaona?

121 Aliangalia, kisha akawaangalia wale kumi na wawili, akasema, “Nyinyi pia mwataka kuondoka?”

122 Sasa, wala wao hawangeweza kueleza jambo hilo, lakini kitu Fulani kilikuwa kimewashikilia. Mnaona, walijua! Hapo ndipo Petro aliposema yale maneno yasiyosahaulika, “Bwana, tumeona Maandiko yamethibitishwa na Wewe. Twende wapi? Tunajua ya kwamba Wewe una Maneno ya Uzima wa Milele. Wewe Ndiwe Chemchemi ya Uzima. Tumeridhishwa na jambo Hili.”

123 Yesu alisema, “Niliwachagua ninyi kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi.” Mnaona, yeye hakuogopa, na kuwapambapamba, na kubembeleza, na kuwapigapiga mgongoni, na kuwabatiza kwa siri, ama cho chote kile.

124 Yeye—Yeye alikuwa Mungu aliyefanyika mwili duniani. Alikuwa Neno la Mungu lililodhibitishwa. Na wale walioona njaa, walikuja. Wale ambao hawakuona njaa, hawangeweza kuja. Kasema, “Wote alionipa Baba, watakuja.” Unawezaje kuja basi isipokuwa Yeye amekukabidhi, umekabidhiwa Kwake?

125 Sasa angalia, tunaona maskini malkia huyu, hatimaye aliwasili. Yeye hakungojea kama tu hao watu walivyofanya. Wengine wao walimfuata yule malkia.

126 Daima kuna tabaka tatu za watu; waamini, wanaojifanya waamini, na wasioamini. Asiyeamini ataamka na aondoke aende zake; anayejifanya mwamini atasitasita hapo kwa muda mrefu. Pale walikuwepo hao watatu. Asiyeamini, ni huo umati mkubwa wa watu; anayejifanya mwamini, ni hilo kundi lililokuwa la mwisho kuondoka. Lakini kulikuweco na mwamini wa kweli ambaye hakuweza kueleza jambo Hilo; hawakujua neno juu Yake, lakini walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno. Hilo linatosha!

127 Hapo tunampata maskini yule malkia. Alikuwa ameleta chakula kingi sana, mikate mingi sana, na vitu vingi sana. Alileta hema zake na kadhalika. Alitupa vitu hivyo chini kutoka kwenye hao ngamia, na kadhalika, huko uwanjani, uani mwa lile hekalu. Naye akapiga hema zake, naye alikuwa akae pale mpaka atakaposhawishika kama ni kweli ama ni uongo.

128 Hapana shaka, siku baada ya siku, alikuwa amesoma hayo Maandiko. Usiku, wao labda walilazimika kusafiri usiku. Mchana, basi angeketi chini ya hiyo mitende, mahali penye chemchemi jangwani, na kusoma yale Yehova aliyokuwa, yale aliyopaswa kuwa. Sasa yeye angemjua Yehova. Kama Yeye alikuwa ndani ya mtu huyo, angejua matendo Yake, angejua kama ilikuwa kweli ama si kweli. Kwa hiyo yeye alikuwa ameyafahamu sana Maandiko.

129 Yeye hakuenda kule na kusema, “Sasa, kama akisema jambo lo lote tofauti na yale kuhani wangu asemayo, nitawachukua tu ngamia wangu niende zangu.” Yeye alikuwa anataka kukaa mpaka atakaposhawishika.

130 Loo, laiti wanaume na wanawake wangalifanya jambo hilo leo! Kuyachukua Maandiko, waone kama Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya leo, ama sivyo, waone kama mambo haya tunayonena habari zake yamebashiriwa kwa ajili ya saa hii tuliyomo. Lakini yeye aliona; hiyo ndiyo sababu Yesu alisema ya kwamba jina lake haliwezi kukosea. . . si haliwezi kukosea, bali ni la milele. Yeye atasimama Siku ya Hukumu na kuuhukumu Dallas, Texas. Ataihukumu Marekani, katika Siku ya Hukumu. Kwa kuwa yeye

alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Yesu Kristo aliyefufuka yuko hapa katika nguvu za kufufuka Kwake. Angalia.

¹³¹ Basi akapiga hema zake. Ninaweza kuwazia asubuhi hiyo, kwa ajili ya watoto sasa. Kengele zikalia, tarumbeta zikapigwa, kanisa likaanza. Walikuwa wakienda kanisani kila siku. Wazia jambo hilo, walipenda kwenda kanisani kila siku. Kwa hiyo wao, kanisa lilianza, ningeweza kuwazia maskini malkia yule alienda huko nyuma kabisa akaketi. Na baada ya kitambo kidogo tarumbeta zote zikapigwa, nyimbo zikaimbwa, na kila kitu.

¹³² Baada ya kitambo kidogo, Mchungaji Sulemani akatokea, akaketi chini. Jinsi watu wote walivyomheshimu, kwa sababu walimpenda. Yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Nao wakatoka, hapakuwepo na hata mmoja aliyekuwa anasema, “A-ha! Laiti angalikuwa *hivi*, laiti angalikuwa wa kundi langu!” La. Kulikuweco na kundi moja tu, na hilo lilikuwa— hilo lilikuwa ni wao wenyewe, kwa hiyo walikuwa hapo.

¹³³ Na basi tunaona, mtu fulani akatokea. Na muda si muda wajua, Sulemani akafunua siri ya mioyo yao. Ningewazia maskini yule malkia alisema, “Sasa ngoja kidogo,” mnaona. “Jamani, hilo lilionekana kuwa ni halisi.” Mwingine akaja, akaona jambo lile lile. Loo, maskini moyo wake ukaanza kupigapiga. Yeye, yeye akashangaa.

¹³⁴ Kwa hiyo hapana budi alipata kadi ya maombi, akangojea. Samahani kwa tamshi hilo; lakini, mwajua, ni kusudi tu niseme jambo muhimu, mnaona. Huenda yeye alipata kadi, kisha akangojea. Siku moja kadi yake ikaitwa, ndipo akaja mbele ya Roho Mtakatifu aliyekuwa akitenda kazi kupitia kwa Sulemani. Nayo Biblia ilisema, “Hakuna kitu kilichofichwa Sulemani.” Roho Mtakatifu aliye mkuu alifunua kila kitu alichohitaji kusikia; akamfunulia.

¹³⁵ Na Roho Mtakatifu alikuwa hapo, utimilifu Wake katika Yesu Kristo, akifanya jambo lile lile; na hao Mafarisayo wakisema, “Tuonyeshe ishara. Mponye mtu *huyu* hapa. Fanya *hivi*, na sema *hivi*. Na jambo *hili* litakuwa vipi, ama *lile*? Mnaona, wao hawafahamu tu.

¹³⁶ Maskini malkia huyu akiwa amesimama pale, nayo Biblia ilisema ya kwamba, “Hakuna kitu kilichofichwa Sulemani.” Yeye alifunua mambo yote aliyokuwa na haja ya kujua. Alimwambia mambo yote.

¹³⁷ Na wakati jambo hilo lilipotendeka, haikumbidi kuchukua neno la mtu mwingine, alikuwa ameliangalia na kuliadini. Ndipo akawageukia wasikilizaji, na kusema, “Yote niliyosikia, wakati niliposikia jambo hilo, nilishangaa. Lakini yote niliyosikia ndivyo yalivyo, na hata zaidi ya nilivyosikia ndivyo ilivyo.” Unaona, ilikuwa ni zamu yake, alikuwa ameona jambo

hilo. Lilitendwa juu yake. Alijua ilikuwa ni ya kweli. Naye akasema, “Abarikiwe Bwana Mungu Ambaye amekufanya mtumishi Wake. Abarikiwe . . .”

¹³⁸ Ilikuwa ni kitu gani? Maskini mwanamke huyo alikuwa ameishi pale, kanuni hizo zote za imani na sanamu, na wakati mmoja katika moyo wake wenye njaa . . . Mwamini ye yote aliye halisi anataka kumwona Mungu katika matendo. Kama yeye alipata kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Naye aliona jambo fulani lililokuwa halisi, si la kuigiza; halisi kabisa. Yeye akamtumikia Mungu siku zake zote zilizosalia, kwa kuwa aliona jambo fulani lililokuwa halisi.

¹³⁹ Loo, ewe rafiki, tumeona wengi sana, “Jiungeni na kanuni hii ya imani, Mwislamu huyu, *hili*,” cho chote kile, “njoo kwenye *hili*, na *hili*, *lile*, na *lingine*,” na kila namna ya miamsho na kadhhalika. Hakika ulimwengu unapaswa kuwa na njaa usiku wa leo kwa ajili ya jambo lililo halisi, kuona jambo lililo halisi. Si kundi fulani la hadithi za kutiririka damu, ama mikwaruzo, ama mafuta, au kitu fulani ambacho hata si cha Kimaandiko; lakini Yesu Kristo halisi Ambaye aliahidi ya kwamba angeishi katika watu Wake katika siku hizi za mwisho, na kufanya mambo aliyofanya, jambo fulani ambalo Maandiko yanasema yangetukia katika siku hizi za mwisho.

¹⁴⁰ Kanuni hizi zote za imani, “Vema, kama unajua kanuni zetu za imani, unajua.” Unaona, wewe—wewe—wewe unaangalia kule nyuma kwa yale Bw. Luther aliyosema, mtu aliyekuwa mkuu katika siku zake. Hakika. Si zaidi ya baadhi ya hawa wanawake hapa, wenye umri wa miaka sabini na mitano, wakijaribu kuwa na umri wa miaka kumi na sita, wakiangalia nyuma na kujaribu kuvaa kana kwamba wao ni wa miaka kumi na sita, wanakata nywele zao na kuvaa kaptula, na kufanya . . . Mtu ye yote anayeendesha gari, huku anaangalia kwa kioo cha nyuma, hupata ajali ya barabarani. Na hiyo ndiyo shida ya kanisa leo, linaangalia kwa kioo cha nyuma, kuona lilivyokuwa. Si ajabu limepata ajali ya barabarani likaangamizwa. Usininii kamwe . . .

¹⁴¹ Paulo alisema, “Tukipiga mbio tuifikilie mede ya Wito mkuu, nakaza mwendo. Nakaza mwendo.” Najua Bw. Moody alikuwa mtu mashuhuri, Bw. Wesley alikuwa mtu mashuhuri, ufufuo wa Kipentekoste, ufufuo wa Kibatisti, ilikuwa mikubwa, lakini hebu na tupige mbio tuifikilie mede ya Wito mkuu katika Kristo. Usiangalie kwa kioo cha nyuma, miaka arobaini iliyopita. Angalia yale usiku wa leo. Angalia yale Maandiko yanayoahadi usiku wa leo. Yeye aliyaahidi katika siku ile, lakini tunaishi juu zaidi ya mahali hapo sasa. Tunasonga mbele.

¹⁴² Na kama Wesley angaliangalia nyuma na kuona yale, Luther, unaona? Lakini hakuangalia aliyosema Luther, aliangalia yale Mungu aliyosema. Vipi kama Wapentekoste

wangeangalia nyuma kwa Wamethodisti? Mnaona mahali ambapo mngalikuwa? Naam basi, jambo lile lile, mlifanya madhehebu mkalizuia, hamwezi kusogea mahali po pote. Sasa Roho wa Mungu anaondoka moja kwa moja, anaenda mahali pengine.”

¹⁴³ Kila wanapofanya jambo hilo, mpango wa binadamu ambapo ninyi nyote huchochewa namna hiyo, inakuwa tena kama yale maasi ya Kora, jinsi Dathani na hao wote walivyotaka kupata kundi kubwa la watu na kufanya madhehebu kutokana nalo. Mungu akasema, “Jitenge, Musa, kutoka kwao, nami nitawameza moja kwa moja ardhini.” Na huo ulikuwa ni mfano wa ile safari leo, nanyi mnajua jambo hilo, barabarani kwenda katika nchi ya ahadi. Na wao walikuwa pale. Hawangeweza kuamini ya kwamba ujumbe ule wa Mungu uliotiwa mafuta, uliokuwa unasonga mbele moja kwa moja, nao walitaka kuanzisha jambo fulani wenyewe. Daima imekuwa namna hiyo.

¹⁴⁴ Kosa baya sana walilopata kufanya Israeli, ni wakati walipoikataa neema, katika kutoka 19, na kuchukua torati. Naye Dathani alifanya kosa baya sana alilopata kufanya, wakati yeye aliposema, “Kuna viongozi wengine hapa mbali na wewe, Musa.”

¹⁴⁵ Na—naye alikuwa amethibitishwa ya kwamba alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Alikuwa amechukua mavumbi akayageuza yakawa viroboto. Na kila kitu alichokuwa amesema kilitimia. Naye Mungu alikuwa pamoja naye. Nguzo ya Moto ilikuwa imemthibitisha, ikining’inia juu yake pale, nao wangali walitaka kuanzisha kitu kingine. Hilo ni la kujibunia tu.

¹⁴⁶ Hivyo ndivyo ilivyo leo. Hapo ndipo kanisa lilipofikia. Hiyo ni kweli. Loo, enyi kanisa la Mungu aliye hai, hamtaki kuona kitu ambacho ni halisi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jambo lililo halisi!

¹⁴⁷ Hadithi fupi kabla hatujawaombea wagonjwa. Ninapenda kuwinda. Mama yangu, mwajua, ni...yeye...mama yake alipata ujira wa kustaafu. Alikuwa Mhindi wa Cherokee. Mimi...na kuongoka kwangu hakukuondoa upendo wangu wa mwituni. Napenda misitu. Huko ndiko unakomwona Mungu. Huko ndiko nilipomwona Mungu kwa mara yangu ya kwanza, ilikuwa ni huko mwituni. Huko ndiko anakokutana nasi. Huko ndiko anakozungumza. Huko ndiko wale Malaika saba walikokutana. Ulijua...kwenye, *Mabwana, Ni Wakati Gani?*

¹⁴⁸ Mimi na Ndugu Borders tulikuwa tumeketi pale majuzi, wakati (nikisimama) uliposhuka, upepo wa kisulisuli kutoka mbinguni, hata ukaiapasua miamba, papo hapo juu mahali pale nilipokuwa nimesimama, yale Yeye aliyosema, unaona. Na pale, loo, watu wengi, Ndugu Sothmann ndani hapa mahali fulani, mmoja wa...Terry, hapa ninaamini, alikuwepo wakati huo. Na mambo, mliyoayaona huko nyikani kule nje! Ninapenda kuwinda.

Ninafanya jambo hilo tu nipate kutoka nje, si kwa ajili ya kuua wanyama pori, lakini nipate tu kuwa mwituni.

¹⁴⁹ Nilikuwa na mazoea ya kuwinda pamoja na jamaa mmoja kule juu New York, huko katika New Hampshire, hasa, yeye alikuwa mwi—mwindaji hodari. Jina lake alitwa Bert. Alikuwa ni Mwingereza. Na ninii wake, wazazi wake ndio walioanzisha, ama kukata hapo, mahali wanapoita Jefferson Notch, kupitia kule, na huko Corroll Notch, na kuitenganisha hiyo katika siku za mwanzoni. Aliishi na kijana mdogo wa Kihindi, pia. Lakini alikuwa mtu mwenye shabaha sana niliyepata kumwona, na mmoja wa wawindaji hodari sana. Haikukubidi kuwa na wasi wasi kuhusu kutoka na kwenda pamoja naye kuwinda; yeye alijua mahali alipo. Nilipenda sana kuwinda kulungu mwenye mkia mweupe kule juu. Nao . . . Nami ningekwea kule kila majira ya kupukutika majani na kuwinda.

¹⁵⁰ Yeye alikuwa ni mwindaji hodari sana, lakini alikuwa ni mtu mkatili sana niliyewahi kukutana naye maishani mwangu. Alikuwa na macho kama ya mjusi, naye alininii tu . . . Macho ya namna hiyo, mwajua, kama vile ya wanawake wanavyojaribu kujipaka rangi machoni mwao siku hizi, kama ya mjusi. Vema, kwa kweli alikuwa na jicho la namna hiyo. Nayo hayaonekani kama ya mwanadamu, kwangu mimi. Na kwa hiyo mimi—mimi daima kwa namna fulani nilichukia kumwangu. Yeye alikuwa anaonekana kama anakirihisha, mwajua, ukiyaangalia hayo macho upande.

¹⁵¹ Basi alikuwa bahili sana. Naye angewaua watoto wa kulungu, hao ni watoto wadogo wa kulungu, mradi tu anifanye mimi nijisikie vibaya. Naye angesema, “Loo, ewe mhubiri, wewe ni kama wengine wao. Wewe ni mwoga sana. Ungalikuwa mwindaji bora kama usingekuwa mhubiri.”

¹⁵² Nikasema, “Mimi ninawinda nafsi, Bert.” Nami nikasema, “Una moja iliyopotea.”

¹⁵³ Naye, “A-ha, jirudie!” Kasema, “Billy, wewe huna shida, lakini,” akasema, “Usinizungumzie upuuzi kama huo.” Kwa hiyo yeye—yeye angewaua hao watoto wa kulungu, na—na jambo hilo lilinifanya tu nijisikie vibaya sana.

¹⁵⁴ Sasa ni sawa kuua ndama wa kulungu kama sheria inasema jambo hilo, sasa, ukubwa wala jinsia, lo lote lile sheria isemalo. Nilikuwa mlinzi wa wanyama pori kwa miaka mingi. Lakini angalia, Ibrahimu alichinja ndama na kumlisha Mungu, kwa hiyo kuua ndama wa kulungu si kitu, endapo sheria inasema hivyo. Lakini si kuwaua ovyo, kuwaacha wamelala hapo tu, na kujivunia jambo hilo; hilo ni kosa, kufanya hivyo si halali. Kwa hiyo nilisema tu jambo hilo kuwahesabia haki ndugu zangu wawindaji walio hapa, mnaona, ili kwamba mpate kuona ninalojaribu kumaanisha.

155 Sasa angalia jambo hili, ya kwamba tunaona ya kwamba mtu huyu. Siku moja nilipanda nikaenda kule, nilikuwa pamoja na mke wangu. Na—naye akajitengenezea filimbi ndogo iliyolia na kusikika kama ndama mchanga wa kulungu anayelia, mnajua, mlio mdogo wa ajabu wanaofanya. Vema, mradi tu . . .

156 Nilikuwa nikifanya kazi, nami sikuwa nimemaliza katika wakati mzuri, katika mkutano, nami nikapanda nikaenda kuwinda pamoja naye. Na kulikuweko na kuwinda kwingi kulikokuwa kukiendelea, na mara ya kwanza tu bunduki inapolia, katika nchi hiyo, hao mikia myeupe. . . U—ulifikiri Houdini alikuwa hodari kwa kutoroka; yeye alikuwa ni mchezo, kwao. Kwa ghafla, wote wangejificha. Na kama kuna mbalamwezi, wao wangekula nyasi usiku; ama wajifiche chini ya fungu la kichaka ama cho chote kile, nao—nao hawangesogea.

157 Ndipo tunaona siku hiyo, nikasema, “Bert, hu—hutatumia filimbi hiyo?”

158 Akasema, “A—ha, ewe mhubiri, wewe ni mwoga sana!” Kasema, “Jirudie.”

159 Ndipo tukaanza kwenda, na tuliweka sambusa kwenye shati—kwenye shati letu. Na tulikuwa tukiwi- . . . tulikuwa tuwinda mpaka kwenye kama adhuhuri, huko juu kwenye mzingo wa—wa Safu ya Milima ya Presidential, kisha tutengane na tutelemke chini tukirudi. Kama tulipata kulungu ye yote, tunajua mahali angekuwa ananing’inia, tungekwenda tukamchukua, katika siku moja ama mbili; tumtundike. Kwa hiyo kulikuwa na kama, loo, inchi nne za barafu, ama sita, kitu kama hicho, ulikuwa ni wakati mzuri wa kufuatia nyayo. Nasi tukaanza kwenda, tukafikia karibu, mlimani, hapakuwepo na mburuzo, hapakuwepo na kitu. Mwezi ulikuwa ukiangaza usiku, na kulungu. . . [Mahali patupu—Mh.]

160 Bert alikuwa mbele yangu, akiongoza njia, na kwa hiyo nilikuwa nikitembea nyuma yake. Naye kwa namna fulani akaketi tu chini, namna *hiyo*. Theluji ilikuwa kavu. Ndipo akanyosha mkono wake nyuma akachukue kitu fulani, nilifikiri alikuwa anataka kula sambusa nasi tungepangukana tu kutoka hapo, kwa maana tulikuwa sasa huko juu sana mlimani wakati huo. Naye akanyosha mkono akaurudisha *huku*.

161 Ndipo nikaanza kuchukua sambusa yangu, na nikaanza kutafuta mahali pa kuweka bunduki yangu chini. Basi—basi nikaanza kuchukua sambusa yangu, kisha nikaangalia huku na huko.

162 Akatoa filimbi hii ndogo. Hiyo, nikafikiri, “Jamani, huo ni mchezo mchafu wa hila kufanya jambo hilo.” Kwa hiyo akatoa filimbi hii ndogo, kisha akaniangalia, kwa hayo macho ya mjusi, na kunitazama. Akaiweka ile filimbi ndogo mdomoni mwake, namna *hiyo*. Nikasema, “Bert, hutafanya jambo kama hilo, si vyoyote?”

¹⁶³ Akasema, “Loo,” na akaipulizia namna hiyo. Na, nilishangaa, yapata yadi hamsini kutoka nilipokuwa, upande huo mwingine tu, jike kubwa mno la kulungu likasimama. Sasa, jike la kulungu ni mama kulungu. Naye huyo hapo, macho yake makubwa ya hudhurungi, na maskio hayo yamesimama. Unaona, alisikia. Sasa, yeye alikuwa ni mama, unaona, na mtoto wake mchanga alikuwa analia. Na kwa hiyo haidhuru kama hao wengine walitoka ama hawakutoka, kulikuweco na jambo fulani ndani yake. Yeye alikuwa ni mama.

¹⁶⁴ Kwa hiyo Bert akaangalia namna *hiyo*, kisha akaipiga tena pole pole sana. Na huyo kulungu akatoka moja kwa moja mahali pa wazi. Sasa hilo si jambo la kawaida, si la kawaida kabisa, kujitokeza nje namna hiyo. Naye alikuwa akiangalia pande zote, huku ameinua kichwa chake kikubwa, na macho yake yakitazama kila upande.

¹⁶⁵ Baada ya kitambo kidogo, wakati huyo mwindaji alipounyosha mkono wake na kuchukua ile bunduki, yeye alimwona huyo mwindaji. Kwa kawaida wao watatoweka kama umeme, na wameenda, na mnajua jinsi ilivyo, upesi. Lakini, unajua, yeye hakusogea kamwe. Yeye alisimama tu na kumwangukia, kiubavu-ubavu, alikuwa amegeuza kichwa chake na kumwangukia. Jamani! nikawaza, “Bert, huwezi kufanya jambo hilo.”

¹⁶⁶ Unaona, yeye hakuwa akiigiza jambo fulani. Hakuwa akitenda kinafiki. Hakuwa anaigiza. Yeye, kwa kuzaliwa, alikuwa ni mama. Na mtoto huyo mchanga, sijali kama jambo hilo lilimgharimu maisha yake, alikuwa katika shida, alikuwa akijaribu kumpata mtoto huyo. Alikuwa katika shida. Yeye alikuwa, kwa silika iliyo ndani yake, yeye alikuwa ni mama. Naye alimwona yule mwindaji. Lakini akili yake haikuwa kwa mwindaji, ilikuwa kwa ndama wake mchanga aliyekuwa katika shida, ndama huyo mdogo wa kulungu.

¹⁶⁷ Na kwa hiyo akafungua kidude cha usalama kwenye hii ya thelathini-sifuri-sita. Loo, yeye alikuwa mwenye shabaha hodari sana. Akailenga hiyo bunduki vizuri. Ni— nikageuza tu kichwa changu. Sikuweza kuangalia. Si— sikuweza kumwangukia. Kafikiri, “Dakika chache tu zaidi, naye ataulipulia mbali moyo wake wenye upendo sana; akijaribu kupata mtoto wake mchanga, yuko katika shida, akijua ya kwamba huyo mwindaji amelala pale kichakani.” Naye angeulipulia mbali huo moyo wenye upendo sana, akiwa na hiyo risasi ya kipimo cha mia-na-themanini mle ndani. Nami ni—ni. . . Yeye alikuwa na shabaha hodari sana. Akalenga. Nikawaza, “Siwezi hata kidogo kusimama na kuangalia jambo hilo.” Nikampa kisogo.

Na—nami—nikasema, “Bwana, msaidie, ili kwamba asifanye jambo hilo.”

168 Ni—nilisikitika sana. Maskini mama huyo amesimama pale, akimtafuta mtoto wake mchanga, nami nilijua yeye hakuwa akiigiza jambo hilo. Yeye alikuwa ni mama halisi. Yeye angeweza kukimbia, wakati mwingine wo wote. Hangaliamka, wakati sisi tunapita. Lakini kulikuweko na jambo fulani ndani yake.

169 Nami nikangojea, na kungojea, wala bunduki haikupiga. Vema, nikashangaa, “Kuna nini?” Nami nikangojea, kisha nikageuka pole pole sana. Nami nilimwona yule kulungu amesimama pale, angali anamwangalia. Na nikaangalia ule mtutu wa bunduki, ulikuwa unafanya *hivi*. Yeye alininii tu... alikuwa akijaribu kulenga, naye hakuweza kufanya hivyo.

170 Akatupa hiyo bunduki chini ardhini, na akaniangalia mahali nilipokuwa, na hayo macho makubwa yalikuwa yamebadilika. Machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake. Akanikamata kwenye mguu wa suruali kwa nguvu, akasema, “Billy, niongoze kwa Yesu huyo unayenena habari zake.”

171 Ilikuwa—ilikuwa ni nini? Yeye aliona jambo fulani halisi. Unaona? Maskini mama huyo wa kulungu ilimbidi kuonyesha upendo, upendo halisi ambao ulimfanya mwindaji huyo mkatili hapo... aliyekuwa na moyo mbaya sana niliowahi kuona. Si mahubiri niliyohubiri. Ilikuwa ni kile alichooona, kitu fulani kilichokukuwa halisi. Halikuwa jambo la kuigiza. Haikuwa ni kujisingizia. Huyo alikuwa ni mama halisi akimtafuta mtoto wake mchanga, na jambo hilo likamwongoza kwa Kristo. Yeye ni shemasi wa kanisa kule sasa, Mkristo mzuri sana, kwa sababu aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza. Hakikuwa ni kujifanya. Kilikuwa ni halisi.

172 Loo, ndugu, dada, laiti kanisa hili, laiti watu hawa, usiku wa leo, laiti mimi na wewe! Kuna jambo fulani halisi, si la kuigiza. Unaweza kuona wengine wakiigiza, lakini kuna jambo lililo halisi. Kuna kitu fulani ndani ya mtu kinachomfanya amwishie Mungu. Kuna Roho Mtakatifu halisi usiku wa leo, ndugu, ambaye si wa kuigiza. Kule, ni jambo halisi.

173 Na ni wangapi ndani hapa wangetaka kuwa Wakristo vivyo hivyo, na waaminifu kwa Kristo, mauti, mateso, cho chote kile, ungependa kuwa Mkristo kama vile yule kulungu alivyokuwa mama? Ungetaka, hivi hungetaka kuwa namna hiyo? Ningetaka sana kuwa Mkristo wa namna hiyo. Kwamba hata kama maskini yule mwanamke Msirofoinike jana usiku, alikuwa Mkristo wa namna hiyo. Maskini malkia huyu tunayenena habari zake usiku wa leo, alikuwa Mkristo wa namna hiyo; alipoona jambo fulani lililokuwa halisi, alikuwa tayari. Mungu na atasaidie, usiku wa leo, kupokea kitu fulani kilicho halisi, Kristo.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo, tunapoomba.

174 Sasa sijui, ndani ya jengo hili, usiku wa leo, kama kuaninii... kama kuna mtu ye yote hapa, huku mmetulia kabisa, kama kuna mtu ye yote hapa ambaye angetaka, nawe

humjui Kristo kama Mwokozi wako binafsi, na ungetaka kumjua Yeye kama Mwokozi wako, je! ungeinua mkono wako? Mmoja, wawili, watatu. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

¹⁷⁵ Sijui kama kuna wengine hapa usiku wa leo, ambaye amedai kuwa Mkristo, labda ni mfuasi wa kanisa zuri, wa kundi kubwa la watu, lakini hata hivyo unajua ndani kabisa ya moyo wako kwamba huna Ukristo ndani ya moyo wako, uliozaliwa ndani humo. Kama tu yule mama alivyokuwa, kulungu, alizaliwa apate kuwa mama; yeye alikuwa mama, kweli kweli. Nawe ungetaka kuwa Mkristo halisi, kama maskini yule mama kulungu alivyokuwa mama; ungetaka kuinua mkono wako, useme, “Niombe, Ndugu Branham”? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Kila mahali, huko juu kwenye roshani, ninaona mkono wako.

¹⁷⁶ Baba wa Mbinguni, sikujua hata kidogo, kwenye ile siku ya Novemba yenye baridi, nikiwa nimesimama pale, barafu kote kote kwenye shingo yangu, nimelowa maji, kumwona mtu huyo amelala pale, jinsi nilivyozungumza naye, nikaushika mkono wake, nikalia pamoja naye, lakini nikamwambia kuhusu Biblia na kila kitu. Naye akasema, “Loo, labda wewe uko sahihi.” Lakini kuona ilibidi Wewe utume kitu fulani ambacho ni halisi sana, kwamba katika njia ya maumbile ya asili kabisa, ya kwamba ya—ya—ya kwamba hangeweza tu kujizuia kuona ya kwamba kulikuweco na kitu fulani kilicho halisi. Na sasa yeye ni mtumishi Wako, Bwana.

¹⁷⁷ Sasa kuna wengi hapa usiku wa leo. Wengine wao waliinua mikono yao, Baba, ya kwamba hawajapata kamwe kuwa Wakristo, nao wanataka kuwa Wakristo. Mungu, tafadhali usiwaache wawe mmoja wa hawa, wanaokimbia tu na kujiunga na kanisa, ama kuchukua desturi fulani ama kanuni ya imani, ama ubatizo. Lakini hebu na uzaliwe ndani yao, Kristo.

¹⁷⁸ Na hao ambao wamejiunga na kanisa, wao, wanatafuta, Bwana, labda kama maskini yule mwanamke, maskini malkia yule tumekuwa tukinena habari zake. Yeye—yeye alikuwa akiona njaa kwa ajili ya jambo fulani. Na—na wao wanaona njaa, pia, Bwana. Na alipoona kitu fulani kilichokuwa halisi, ambacho kilimtambulisha Mungu katika wanadamu, alikuwa tayari wakati huo. Naye akasema, “Abarikiwe Bwana Mungu wa Israeli!” Hakutaka uhusiano wo wote na taratibu za kipangani tena.

¹⁷⁹ Na, Baba, wengi hapa usiku wa leo, hapana shaka, wako katika hali ile ile. Laiti wanaliona tu jambo fulani lililo halisi! Nawe ulitwambia ulipokuwa hapa ulimwenguni, mambo ambayo yangetukia katika siku hii. Tunaambiwa ya kwamba Wewe ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Nasi tunajua jinsi ulivyotambulishwa, na jinsi Mafarisayo walivyoshindwa

kuona jambo hilo. Bwana, makundi yale yale leo yanashindwa kuona jambo hilo, kwa maana wao ni wafuasi wa kanisa, wakijiunga, wakiwa na namna fulani ya kanuni, na kadhalika. Wao, wanashindwa kumwona Masihi, yule Roho Mtakatifu mkuu akijitambulisha Mwenyewe na watu, kama ulivyoahidi Wewe ungefanya.

¹⁸⁰ Tujalie, usiku wa leo, Bwana, ya kwamba kila mmoja wa hawa atatambua na ataona Uwepo Wako. Naomba liingie moyoni mwao, lile fungu la maneno, “Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa usiku wa leo,” huyo ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliyefufuka, aliye tayari kuja na kuongoa, na kufanya upya mioyo, na kuweka ndani yao tukio la kuzaliwa na Mungu. Kama tu yule mama kulungu, jambo ambalo huyo mama kulungu hakuwa na uhusiano wo wote nalo, kwa neema ya Mungu alichaguliwa kuwa kulungu, alichaguliwa kuwa mama, na mama aliye na upendo. Nawe ulitwambia tulichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

¹⁸¹ Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamjalia kila mmoja wa hao walio na mvuto huo mioyoni mwao, kama maskini yule mama alivyofanya, kumpata Mungu, ya kwamba usiku wa leo kutakuweko na jambo fulani halisi litakalotukia, ya kwamba wataona, na kumtumikia. “Kwa kuwa aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁸² Sasa kwa uchaji, kimoyomoyo, kabla tu hatujaja madhabahuni. Tafadhali, mtu asisogee. Iweni tu na uchaji kwa muda kidogo. Hii ni saa yenye uchaji, wakati wenye uchaji. Uamuzi unafanywa. Wengi waliinua mikono yao. Ninaamini mlikuwa waaminifu sana katika jambo hilo, wakati mliposema jambo hilo.

¹⁸³ Sasa, mmesikia kuhusu Biblia, mmesikia kuhusu Yesu, mmesikia Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mmfundishwa ya kwamba Yeye alifufuka tena, na mnafundishwa ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸⁴ Sasa Roho Mtakatifu huyu tunayenena habari zake, je! huyo ni Yesu Kristo? Hakika, Ndiye. Mnaona, Yeye ni Mungu; anajulikana kama Mungu, Roho Mtakatifu. Si Mungu mwingine; ni Mungu yule yule. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, si Miungu watatu; ni sifa tatu za Mungu yule yule, mnaona, Mungu yule yule kwa tabia tatu. Mnaona, kwa maneno mengine, ilikuwa ni kama afisi tatu, unajua; wakati alipotumika kama Baba, halafu kama Mwana. Ni Mungu akijidhili, akishuka kutoka Mmoja Asiyeweza kuguswa (hata kuugusa tu ule mlima, ilisababisha mauti), kufikia mahali ambapo tungeweza kumgusa Yeye katika mwili.

¹⁸⁵ Na sasa Yeye yuko ndani yenu. Yeye aliwatakaswa kwa Damu Yake, apate kuishi ndani yenu. “Siku ile, mtajua ya kwamba

Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Mnaona? Ni Mungu akiwa juu yetu, Mungu akiwa pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Mnaona?

¹⁸⁶ Na huyo ni Kristo, usiku wa leo, Roho Mtakatifu. Ni yeye yule. Nawe ni ninii... Yeye ndiye mzabibu, nanyi ni matawi. Mwaminini Yeye. Na kama Yeye atajitambulisha Mwenyewe, usiku wa leo, kuwa miongoni mwetu!

¹⁸⁷ Sasa kama angalisimama hapa akiwa na makovu, huyo angekuwa ni mwanadamu, huo ni mwili. Mtu ye yote anaweza kuiga jambo hilo; mwanadamu anaweza kujiumbua. Ama, labda, hatujui sura ya Yesu, tunaninii tu wa—wa—wazo la wanasanaa, saikolojia yake, jinsi sura Yake ilivyokuwa; Hofmann alikuwa na ya namna fulani, Sallman nyingine, na ni wangapi zaidi!

Lakini mngemjuaje? Ingekuwa ni Maisha Yake.

¹⁸⁸ Kwa sababu, kama mtu angalisimama hapa akiwa na makovu ya miiba mkononi mwake, na cho chote kile, huyo angekuwa ni mwigaji; maana, Wakati Yesu Mwenyewe atakapokuja, kila jicho litamwona, kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri hilo. Hakika.

¹⁸⁹ Lakini Roho Wake yuko hapa, mnaona. Kama tunaweza tu kuacha nia zetu ziingie ndani ya nia Yake. “Iweni na nia iliyokuwemo ndani ya Kristo.” Yeye ni Neno. Nayo Biblia ilisema, “Neno la Mungu.” Ambalo, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Neno? Katika Biblia, Waebrania 4, na Biblia ilisema, “Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na Mpambanuzi wa mawazo ya moyo.” Sasa, hilo ndilo lililokuwemo ndani ya Sulemani, (Neno, Mungu) sababu yeye aliweza kutambua mawazo yao. Hilo lilikuwa ndani ya Yesu, unaona. Hilo ndilo lililopo hapa sasa, Jambo lile lile.

¹⁹⁰ Sasa ninyi mlio kule nje. Sitaitisha mstari wo wote wa maombi, kwa maana nitafanya wito wa madhabahuni. Huenda kukawa na wengine hapa ambao hawajawahi kuwa kwenye mmoja wa mikutano hii. Sioni mtu ye yote humu jengoni, ambaye ni—ninamjua.

¹⁹¹ Mtu fulani alikuwa akiniambia ya kwamba walikuwa kama thelathini jana usiku, ama zaidi, walioitwa. Je! unatambua ya kwamba wakati mmoja mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akageuka, na jambo lile lile likatukia, na—na nguvu zikamtoka, Yeye akiwa ni Mwana wa Mungu? Lakini Yeye alisema, “Zaidi ya hii mtaifanya, kwa maana ninaenda kwa Baba Yangu.”

¹⁹² Sasa aminini tu na mwe na imani, kila mmoja wenu, wote waliopo hapa, katika hivi vitanda vidogo, machela, po pote mlipo. Aminini! Msifikiri ya kwamba ninyi hamna matumaini.

193 Sasa kama ningeweza kukuponya, ningefanya jambo hilo, lakini siwezi kukuponya. Ninaweza kukuwekea mikono, na ninakusudia kufanya jambo hilo, kwa kila mtu aliye na hizo kadi. Nao wanasambaza kadi kila siku. Kwa hiyo mimi ninataka kufanya hilo, lakini hivyo ni, hivyo, hivyo ni kuonyesha tu ya kwamba ninaamini pamoja nanyi.

194 Lakini, angalia, kwa nini wewe usimguse Yeye? Biblia ilisema, “Yeye ni Kuhani Mkuu,” sasa hivi, “anayeweza kuchukuana nasi katika hali yetu ya udhaifu.” Hiyo ni kweli? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu, basi bila shaka angetenda kwa njia ile ile aliyofanya wakati huo. Sivyo? Bila shaka angetenda vile vile alivyotenda wakati huo. Vema, sasa wewe mguse kwa imani.

195 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, mkutano ni Wako. Lakini nimefundisha usiku wa leo juu ya maskini mwanamke huyu kuona jambo lililokuwa halisi, wakati alipoona hiyo roho ya utambuzi kwa Sulemani. Nasi tuna hakika, Bwana, ya kwamba Maneno Yako ni ya kweli. Ulisema jambo hilo lingerudi tena, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kabla tu ya kule Kuja; Nawe ulikuwa ni Wewe yule jana, leo, na hata milele. Kazi ulizozifanya Wewe, tutazifanya pia. Nawe ni Kuhani Mkuu, usiku wa leo, anayeweza kuchukuana nasi katika hali yetu ya udhaifu. Tunahitaji kiasi gani zaidi?

196 Hao Wayahudi walihitaji kiasi gani, kuona ya kwamba Yeye alikuwa Nabii? Bikira alipata mimba, na mambo haya yote, lakini, wao, kanuni zao za imani ziliwapofusha.

197 Bwana, kuna wengine hapa waliokuja kama ninii, labda si kutoka Sheba, lakini wamekuja kutoka mahali pengi. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utajitambulisha Mwenyewe usiku wa leo, kweli kweli. Halafu ujitambulisha Mwenyewe ndani yao, kama vile ile silika ya mama yule katika maskini yule kulungu ilivyotenda siku ile. Sisi ni Wako, Baba. Nena kupitia kwetu, katika Jina la Yesu. Amina.

198 Sasa ninawatakeni mwe na imani na mwamini, kila mmoja wenu, kila mahali. Na mwombe tu. Sasa msininii... Sasa angaliani na mwombe sasa, na mwamini tu. Mnaona, jambo hili huenda lisininii, Roho Mtakatifu huenda asifurahishwe na kufanya hili. Kama yeye hafurahi, nitafanyiza mstari wa maombi. Lakini simameni tu hapa. Mtu fulani pale nje, hata kama wewe... Siwataki ninyi mlilo na kadi za maombi. M—mtu ye yote tu a—aombe tu. Bila shaka, nisingejua, lakini ninyi ombeni tu na mwone. Semeni tu, “Bwana Yesu, ninajua ya kwamba mtu yule hanijui mimi. Hana anachojua kunihusu mimi, lakini ninajua ya kwamba ninaamini.”

199 Imani yako haifahamiki. Msisukumane sasa, au kuruka. Utaruka uiache. Iko papo hapo pamoja na wewe. Jitulize tu na uamini. Amini tu sasa, uwe na imani. [Katika kusanyiko, ndugu

fulani anatoa maonyo—Mh.] Amina. Na mwe na uchaji, mwe na imani tu, aminini tu. Wakati mwingine imani yako haifahamiki, unayo na huna habari. Maskini yule mwanamke alikuwa nayo; yeye hakujua alikuwa nayo.

²⁰⁰ Ni wangapi wenu waliopata kuona ile picha ya Malaika yule wa Bwana, ile Nuru? Ni, ilichukuliwa papa hapa Texas. Imesambazwa, ulimwenguni kote sasa.

²⁰¹ Lakini unafikiri nini, bwana? Unaamini, wewe uketiye papa hapa pembeni? Ilionekana kana kwamba ulikuwa unaangalia kwa hamu sana. Huenda una kasoro nyingi sana. Una matatizo, mambo mengi. Sasa niliposema jambo hilo, ulipata hisi ya ajabu sana, sivyo? Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. Sasa mimi sikujui kabisa, sikujui. Hiyo ni kweli. Mnajua nini? Ile Nuru ilishuka moja kwa moja juu yako. Mnaona? Hivyo ndivyo ulivyojisikia, kwa namna fulani kujihisi kutamu sana. Nilikuwa nikiiangalia Hiyo, mnaona, ikishuka moja kwa moja chini.

²⁰² Sasa, naam, wewe uko hapa, unataka kuombewa kabla hujaondoka humu jengoni. Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, nawe umeketi pale, nami hapa, ungeamini ni Mungu? Ni ugonjwa wa mshipa wa rihi, moja ya mambo yako makuu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, kwamba jina lako ni nani, sasa umemgusa vizuri kabisa, utaamini kwamba mimi ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Samahani, hilo ni jiwe la kujikwaa kwa watu wengi, mnaona. Mnaamini jambo hilo? Jina lako ni Bw. Sturg. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Amini jambo hilo, na uponywe.

²⁰³ Huyu hapa bibi maskini anayeketi moja kwa moja kule nyuma, mwenye nywele nyeusi, papa hapa kwenye marefu ya kanisa. Naam, wewe. Ulishangaa wakati jambo hilo liliposemwa. Sasa wakati uu huu unaanza kujisikia wa ajabu kwa namna fulani, unaona, kitu fulani kitamu kinachokuzunguka. Kama mtu ye yote ataangalia, kama unaweza kuona kitu Hicho, Nuru kama ya manjano ikishuka juu ya maskini bibi huyo. Sasa shida yake ni, anasumbuliwa sana na maumivu ya kichwa. Hiyo ni kweli. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako namna hiyo. Nami sijapata kumwona, maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Anasumbuliwa sana na kuumwa na kichwa, kama maumivu makali sana ya kichwa, lakini yatakuacha. Amina. Amini jambo hilo. Sasa ninii. . .

²⁰⁴ Kuna mtu anayeketi papo hapo karibu nawe pale, naye ananiangalia moja kwa moja kwa bidii sana, na hiyo Nuru inaelekea moja kwa moja kwake. Naye mtu huyo anasumbuliwa na shida ni ya macho yake. Lakini kama ataamini, Mungu atayaponya hayo macho na kuyafanya mazima. Mnaamini? Vema. Sijapata kukuona maishani mwangu. Mimi sikujui wewe.

205 Aisee, huyo jamaa mdogo anayeketi karibu nawe pale, pia, anaugua ugonjwa wa kichwa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sijapata kumwona mtu huyo, maishani mwangu. Mungu anajua hivyo, unaona. Vema, unaamini.

206 Mtu anayeketi karibu nawe, amevaa miwani, akiangalia huku. Naam, unavaa miwani, lakini hiyo siyo shida yako hasa. Una shida fulani na mgongo wako, ambao unataka uombewe. Kama jambo hilo ni kweli, pepea mkono wako. Vema.

207 Jamaa yule mdogo anayeketi papo hapo karibu kabisa nawe, hapo tu karibu yako. Amekuwa na shida nyingi sana, kijana mwanamume huyo anazo shida. Naam, bwana, aliyevaa tai nyekundu shingoni, umekuwa na shida nyingi sana katika jamaa yako na kadhalika. Kwa namna fulani, mke wako ni aina ya mtu mwenye wasiwasi, nawe unaugua msukumo fulani kichwani mwako, pia. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wewe amini tu. Usitilie shaka, lakini amini.

208 Hapa pana mwanamke anayeketi papa hapa nyuma. Huoni hiyo Nuru inayosogea huko nyuma, nayo inatulia papo hapo? Anaumwa ugonjwa wa macho, kibofu chake. Loo, yeye atalikosa Hilo. Bwana Mungu, nisaidie. Jina lake ni Bibi. Chambers. Amini kwa moyo wako wote, Bibi Chambers. Simama kwa miguu yako. Simama, watu wapate kuona wewe ni nani. Mimi ni mgeni, sijapata kumwona maishani mwangu. Naam. Imekwisha sasa. Yesu Kristo anakuponya.

209 Sasa kama hilo si Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye yuko wapi? Je! yeye aliahidi kufanya jambo hilo? Wote wanaoamini jambo hilo, inueni mikono yenu. Vema.

210 Unataka kuwa Mkristo halisi, ninyi mlioinua mkono wenu muda kidogo uliopita; kama vile maskini yule mama kulungu alivyokuwa? Wakati Roho Mtakatifu yuko hapa, na upako upo kila mahali juu yetu, mbona usije, uje na kusimama papa hapa madhabahuni, kwa muda kidogo tu. Kama unamtafuta Mungu kwa ajili ya wokovu, je! waweza kuja hapa, na uje tu hapa kwenye madhabahu hii na kusimama hapa pamoja nami kwa muda kidogo? Simama. Namna hiyo. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Mtu ye yote jengoni, po pote ulipo, utakuja? Hiyo ni kweli. Njoni sasa hivi, ninyi mnaotaka kutamfuta Kristo.

211 Hutakuwa karibu Naye zaidi mpaka utakapokutana Naye. Yeye yuko hapa. Ametambulishwa, kitu fulani kilicho halisi. Umejiunga na kanisa, wengi wenu wafuasi wa kanisa sasa, mmejiunga na kanisa lakini hayo tu ndiyo mliyokuwa nayo, mnataka kuona jambo fulani lililo halisi. Kama hivyo sivyo hasa Yesu Kristo alivyojitambulisha Mwenyewe kuwa!

212 Mwangalie huyu mtoto mdogo anayeketi hapa, akilia, machozi yakitiririka maskini usoni mwake. Si ajabu, wao ni wachanga. Hawajapitishwa kwenye kila kitu. Mwingine anashuka anakuja kwenye marefu ya kanisa, mwingine kule

nyuma, anashuka, watoto wadogo, wakati watu wazima wamepita wakati wao. Mnaweza kuja? Njoo moja kwa moja hapa sasa na usimame karibu na madhabahu. Ninyi wafuasi wa kanisa, ninyi watu mnaotaka kupata tukio la Kristo moyoni mwenu, mnaweza kuja hapa? Kama Yeye anaujua moyo wako, nawe unajua hungeweza kuuficha, si uje sasa hivi na usimame hapa, kabla tu hatujasonga mbele zaidi. Njoo hapa, msimame hapa tuombe. Mtafanya hivyo?

²¹³ Njoni, onyesha, mtetee Yeye. Mtetee. Kama unaona haya kwa ajili Yake sasa, Yeye atakuonea haya kule.

²¹⁴ Kumbukeni, Yeye yuko hapa. Maandiko yalisema haya yangalitukia, na Yeye hapa akijitambulisha Mwenyewe kwamba yuko hapa. Kama wewe ni mfuasi wa kanisa, nawe humjui Kristo kama tukio halisi, mbona usije wakati huu? Sasa, mimi sijui kuwashawishi watu sana. Jambo pekee ninaloweza kusema, ni kuwaambia Kweli, na Uwepo wa Kristo, pamoja na Neno Lake likidhihirishwa.

²¹⁵ Huko juu kwenye roshani, ninyi mlioinua mikono yenu; dada, ndugu, kama unataka kushuka uje, tutangojea papa hapa. Shuka uje moja kwa moja, muizunguke madhabahu, kwa maombi mafupi tu. Hebu ulimwengu na ujue, hebu Yesu ajue ya kwamba wewe huninii—wewe huoni haya, unataka kuwa Mkristo halisi. Mbona usije, wakati tunapongojea kwa dakika moja ama mbili?

²¹⁶ Mfuasi wa kanisa, uliye vuguvugu, uliyerudi nyuma, mbona usije na kusimama pamoja nao sasa? Njoo hapa na usimame, ninyi ambao hamjafanya hivyo, kama huna tukio na Mungu, ya kwamba umezaliwa katika Ufalme wa Mungu, namna hiyo.

²¹⁷ Unataka kuona jambo gani zaidi? Kumbuka, ninawaambia katika Jina la Bwana, kama mnanihesabu kama mtumishi Wake, hii ndiyo ishara ya mwisho ambayo kanisa litaona, kulingana na Maandiko. Hilo lilikuwa ndilo jambo la mwisho ambalo Ibrahimu aliona likifanyika kabla ya mwana wa ahadi kuwasili. Nasi ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, naye Yesu aliuahidi Uzao wa kifalme kuona jambo lile lile aliloona Ibrahimu, kabla tu ulimwengu wa mataifa haujateketezwa kwa moto. Usiliahirishe kwa ajili ya jambo jingine. Shetani anajaribu kukufanya uangalie huko ng'ambo. Njoo, sasa hivi ambapo . . .

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu
Iliyotolewa kutoka vena za Immanueli,
Ambapo weye dhambi wakitumbukizwa chini
ya mafuriko hayo,
Wanaondokewa na madowa yote ya hatia.

Yule mwivi aliyekuwa anakufa aliyefurahi
kuona
Chemchemi ile katika siku yake;

Pale nijalie mimi, ingawa ni mchafu kama
yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.

218 Mbona usije na kulikubali sasa? Ninangojea kwa muda kidogo tu, mtu mwingine anaweza kuja na kusimama hapa kwa ajili ya maombi.

219 Sasa nitawaomba wahuduma hapa, ndugu, washuke waje na kusimama pamoja nami, hapa, tunapoomba; na wahudumu huko, ambao wanahusika, na baadhi ya watu hapa jirani yenu, ambao wangekuja kanisani mwenu ama—ama cho chote kile, ambao wana—wanapenda wa—watu wamjie Kristo, nanyi mnaamini huyu kuwa ni Yesu Kristo.

220 Sasa, kumbukeni, mimi si Yesu Kristo. Mimi ni ndugu yenu, mwenye dhambi aliyekolewa kwa neema. Mimi niko kama mliyvo ninyi. Lakini ni Yesu Kristo, Roho Mtakatifu aliye hapa pamoja nasi, akitimiza Neno Lake. Si lazima afanye jambo hili, lakini Yeye aliahidi angelilifanya. Haikumlazimu Yesu kuwaponya wagonjwa, lakini Biblia ilisema, “Yeye alifanya hilo, ili yatimie yale yaliyoahidiwa Yeye.”

221 Sasa, hatujali wewe ni mfuasi wa kanisa la aina gani; kama unaamini ya kwamba Yesu Kristo yupo, unaamini ya kwamba kuna tukio la kuzaliwa mara ya pili, la ubatizo wa Roho Mtakatifu.

222 Wahudumu, sogeeni moja kwa moja hapa, kati ya watu hawa hapa. Njoni papa hapa miongoni mwao, mkiweka mikono yenu juu yao. Tutawaomba. Ninaomba kusanyiko letu mwe wenye uchaji mwezavyo kuwa kwa muda mchache. Tunajuaje kile atakachofanya Roho Mtakatifu! Naam, sogeeni moja kwa moja, changanyikeni na watu. Njoni papa hapa karibu yao kabisa, kila mmoja.

223 Sasa kumbukeni, kuna jambo moja tu la kufanya, ni kukubali yale aliyowaahidi. Je! mmeona uhalisi wa kukufuka kwa Kristo?

224 Sasa nitaliuliza kusanyiko kama watasimama kwa muda kidogo, kwa uchaji na heshima kwa ajili yao. Kila mmoja wenu aamini sasa. Ungameni yote mliyofanya, hivyo tu ndivyo mnavyoweza kufanya, kisha mmwombe Mungu awasamehe. Na mkubali jambo hilo, mliamini. Sasa kila mtu na aombe kwa njia yake.

225 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako, na nafsi zenye mawaa. Jinsi hadithi hiyo fupi, kuhusu yule mama kulungu, iliingia kwenye kilindi, kwamba watu walitaka kufanya jambo fulani, ama kuona jambo fulani lililo halisi; kama yule malkia wa Kusini, aliyetoka kutoka pande za mwisho za dunia, kusikia hekima ya Sulemani. Na aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa, Mwokozi wa watu, Yesu Kristo wa Nazareti! Waokoe, Baba. Wasamehe dhambi zao. Safisha nafsi zao katika Damu ya

Mwana-Kondoo, na uwape tukio la kuzaliwa Mkristo. Hakuna mnyama mwingine, hakuna kitu kingine, kingaliweza kufanya jambo hilo, ila mama kulungu. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Tupe tukio hilo, Bwana, sasa, tukio la kuzaliwa mara ya pili, katika Ufalme wa Mungu, wakati Roho Mtakatifu angalipo hapa. Tujalie, Bwana. Tujalie, Bwana.

²²⁶ Sasa fumbeni macho yenu, inueni mikono yenu, na kusema, ungameni, mkisema, “Yesu, sasa naamini. Nitwae jinsi nilivyo. Hakuna jambo lingine niwezalo kufanya. Uponye mwili wangu ulio mgonjwa. Nitwae, Bwana. Ninaamini wewe uko hapa, Roho Mtakatifu yupo hapa akijitambulisha Mwenyewe. Niokoe kwa neema Yako, Bwana. Ndivyo tu ninavyojua jinsi ya kufanya. Katika Jina la Yesu Kristo!”

Ndugu Grant, utatuongoza kwa maombi?



ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA SASA SWA64-0306
(A Greater Than Solomon Is Here Now)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Ljumaa tarehe 6 Machi, 1964, katika Hekalu la Bandari ya Nafsi huko Dallas, Texas, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org